WARNING: SINGLE USER product.

Use of this material is limited to the registered user.

Materials provided on CD NOTES are copyrighted by World Video Bible School® and **MAY NOT** be used, reproduced, distributed, republished, displayed, broadcast, hyperlinked or transmitted, in whole or in part, in any form or by any means, electronic or mechanical including photocopying, electronic transfer, installing on computers, recording or the use of any information storage and retrieval system, outside of the following permitted use limits:

The **REGISTERED USER** may copy the contents of this CD to their hard drive and store the CD as an archive. If using more than one computer (i.e. home & office), you may copy it to each computer.

The **REGISTERED USER** may print unlimited copies of any and all materials contained on this CD, from their computer for personal use or use in teaching classes, provided World Video Bible School® is given proper credit and materials are not resold.

BE ADVISED *that WVBS may, at their sole discretion, employ text marking and detection techniques to identify the original purchaser of pirated electronic or printed copies of this material. More importantly, remember that you will answer to God for every word and action (Matthew 12:36). Please consider your actions carefully and proceed accordingly, with a clear conscience.*

Shule Ya Biblia Ulimwenguni Kwa Njia Ya Kideo

Ilianza 1986

ELIMU YA KUFASIRI MAANDIKO MATAKATIFU

HERMANUITIKSI

Mafunzo haya yametengenezwa ili ya saidie wanafunzi Shule ya Ulimwengu kwa njia ya ya kideo wasiotafuta kutunukiwa, wanaosomea nyumbani kwa kupata cheti. Mwanafunzi atatakiwa kuweka bidii katika mtaala mzima. Mwanafunzi asiyetaka kutunukiwa anaweza asijali kufuata mtaala na kutumia mafunzi apendavyo kwa manufaa yake ya kiroho.

Shule Ya Biblia Ulimwenguni Kwa Njia Ya Kideo
130 Lantana Lane
Maxwell, Texas 78656-4231
Marekani.

biblestudy@wvbs.org
http://www.wvbs.org/

Shule Ya Biblia Ya Arusha
Sanduku la Barua 12163 Arusha
Tanzania.

(ELIMU YA UFASIRI-HERMANUITIKSI)

Mtaala

I. HABARI MUHIMU.

A. Mwalimu: Francis Wechesa

B. Mafunzo haya yana masomo 18

II. KUSUDI YA SOMO HILI

A. Kusoma kwa undani elimu ya ufasiri wa Biblia
B. Tutakazia kujifunza kuhusu mazoea na uhusishaji wa kanuni na utaratibu husika.
C. Mwanafunzi atakuwa na ufahamu wa kutumia zana na mafunzo ya Hermanuitiks yanayofundisha namna ya kufasiri Biblia.
D. Mwanafunzi atafahamu tofauti ya kati imani na ufasiri bora.
E. Mwanafunzi atafahamu hitaji la kujifunza kwa undani Biblia.
F. Mwanafunzi atafahamu namna ya k utambua tafsiri mbaya za maandiko matakatifu.

III. VIFAA VYA KUTUMIA KATIKA DARASA HILI:

1. YATAKIWAYO:
   A. Biblia ya kiswahili
   B. Masomo kutoka kwa mwalimu.

I .YATAKIWAYO:

A. Soma notisi utakazopewa kabla ya kuingia darasani

B. Ongezea yote ambayo mwalimu atakayokuwa akifundisha darasani.

C. Somo madondoa yote na kuwa tayari kuayaandika kila tunapoingia darasani.

D. Ujitayarishe kwa mitihani ya chemsha bongo itakayotolewa na mwalimu kwa wakati atakaoona ni mwafaka.

E. Wastani ya alama za kufaulu ni 70

F. Insha ya mhula(Term paper) irudishwe tarehe 19th June 2001. Utatakiwa kuandika insha yenye kurasa nane.

G. Insha hii itatakiwa kuwa tayari mwisho wa muhula.

IV. MADONDOA

A. Madondoa yanapaswa kuandikwa darasani.

B. Mistari ya kudondoa katika somo la Hermanuitiks ni:

1. Zaburi 1:1-3
2. Zaburi 12:6
3. Mithali 30:5-6
4. Efeso 4:14-15
5. 1Thess. 5:21
6. 2Tim. 2:15

7. 2Tim3:16-17
8. 2Peter 1:20-21
9. 1Yohana 4:1

C. Madondoa yatahitajika kila tunapoingia darasani kuanzia tarehe 30/05/2001

D. Mbinu za rahisi za kudondoa mistari, andika kwenye karatasi.

V. MAJARIBIO:

A. Kutakuwa na chemsha bongo mara kwa mara.

B. Mtihani wa mwisho utatokana na chemsha bongo

VI. KARATASI LA INSHA LA MHULA

A. Katika ukurasa wa tatu kuna orodha kanuni ya kimaandiko kumi inayotumika kama msingi wa kozi ya Hermeneutiks. Andika ukifafanua umuhimu wa kila moja. Toa mifano ya kibiblia ukionyesha namna kila kanuni inavyohusishwa katika Biblia.

B. Karatasi la insha linapaswa kuwa na kurasa kumi

VII. KUSAHIHISHA:

A. Madondoa, karatasi ya insha, mitihani vitahesabiwa tofauti.

B. Alama ya mwisho itategemea wastani wa kazi yote uliyopewa darasani na mwalimu kwa muhula mzima.

MAMBO YA UTANGULIZI

H. Hermanuitics ni sayansi ya utafsiri.

a. Neno lingeni karibu na mafunzo yetu ni “exegesis”

1. Exegesis kama litakavyotumika katika kozi hii ni namna ya kutumia Hermanuitiks(sayansi ya utafsiri)

a. Katika hermanuitiks tunatambua kanuni
(1) 2Tim. 3:16,17)

b. Katika exegesis, tunaziweka kanuni hizi katika matumizi.

2. Kusudi la exegesis ni kuleta nje wazo lililokusudiwa au maana mwandishi aliyokuwa nayo wakati wa kwandika.

c. Umuhimu wa kozi hii, haiwezi ikakadiriwa, kwa sababu ni ya hali ya juu zaidi.

d. Hermanuitiks halisi ni muhimu kwa sababu itatusaidia kuelewa vema yafuatayo:

1. Vitu vya mwisho.
2. Kushauri watu.
3. Maisha ya filosofia
4. Mungu
5. Mwanadamu
6. Dhambi na
7. Wokovu.

II. UTANGULIZI KATIKA MAMBO YA MSINGI KUMI YALIYO MUHIMU KUTUSAIDIA KUFAHAMU MAANDIKO MATAKATIFU.

A. Mtu anapaswa kuwa na imani ya kweli kuhusu mamlaka ya maneno ya liyo vuviwa na Mungu, kama ndiyo mamlaka ya mwisho katika maisha.

B. Mtu anapaswa kufahamu kwamba Biblia sehemu ya Agano la Kale ilitolewa katika lugha ya kiebrania na Agano Jipya katika lugha ya Kiyunani.

C. Mtu anapaswa kukubali sababu ya kimaandiko kwamba Mungu alitupa Biblia inayofahamika, ili tuiamini, na kuitii, na kwa hiyo Mungu anatuadhibisha kuifahamu.

D. Mtu anapaswa kutambua kwamba Maandiko matakatifu hufahamika ukiwa na usikivu wa kiroho sawa na wa akili na elimu.

E. Mtu anapaswa kutafakari juu ya neno la Mungu usiku na mchana.

F. Mtu anapaswa kufahamu kwamba ni lazima kupata kusudi lote la Mungu kuhusu kila somo ili kuweza kupata mapenzi ya Mungu kamili,sehemu ya ukweli hautoshi.

G. Mtu anapaswa kutumia mazingira sahihi katika kila maneno ya maandiko matakatifu.

H. Mtu anapaswa kutambua kwamba, kuna mambo yaliyokuwa ya muda na yale yaliyo kuwa ya kudumu.

I. Mtu anapaswa kufikia uamuzi wa mwisho kutokana na ushahidi uliopo.

J. Mtu anapaswa kufahamu kwamba kuna vitu vigumu katika Biblia kufahamu.

III. MAFUNZO KWA UNDANI KUHUSU MISINGI YA KIMAANDIKO HII KUMI.

A. Mtu anapaswa kuwa na imani ya kweli kuhusu mamlaka ya maneno ya liyo vuviwa na Mungu, kama ndiyo mamlaka ya mwisho katika maisha.

1. Bila hii kanuni zote kuhusiana na hermanuitiks na exegesis hushindwa.
2. Mzungumzo kuhusu ubishi wa marehemu Thomas Warren kuhusiana na Ukristo hapa sasa utahitajika. Alijenga hoja zake ifuatavyo:

a. Ikiwa mwanadamu anaweza kufahamu:

1. Kwamba Mungu yupo,

2. Kwamba Biblia ni neno la Mungu,

3. Kwamba Biblia hufundisha kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu na kwamba kuokolewa kutoka dhambini, wanadamu wanapaswa kuamini katika yeye, k umpenda, na kumtii, basi, wanadamu wanaweza kufahamu kwamba Yesu ni mwana wa Mungu na kufahamu kwamba, ili kuookolewa, kutoka dhambini, wanadamu wote wanapaswa kumwamini, kumpenda, na kumtii.

b. Wanadamu wanaweza kufahamu:

1. Kwamba Mungu yupo,

2. Kwamba Biblia ni neno la Mungu,

3. Kwamba Biblia inafundisha kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu na kwamba kuokolewa kutoka dhambini, wanadamu wanapaswa kuamini katika yeye, kumpenda, na kumtii.

c. Kwa sababu hiyo, wanadamu wanaweza kufahamu kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu. Na kwamba ili kuookolewa, kutoka dhambi zao, wanapaswa kumwamini, kumpenda, na kumtii.

4. Kidokezi kwamba, Biblia haikuvuviwa, haina mamlaka, inamakosa, ni jambo lisilowezekana.

a. Tukishikilia kwamba, Biblia ina maneno ya Mungu na maneno ya mwanadamu, tutalazimika kuelezea ni yapi maneno ya Mungu na yapi ya mwanadamu.

b. Kama Biblia si neno la Mungu, basi haina kanuni ya moja kwa moja kuhusu maisha yetu. Na kwa h iyo, tunajitawala sisi wenyewe kwa kufuata hisia zetu kujua ni lipi jema na baya na kwa njia fulani, tunapaswa kutoa hesabu kwa vitu kama:

(1) Unabii uliyotimilishwa.
(2) Uwiano (Umoja)
(3) Usahihi wa Historia
(4) Usahihi wa kisayansi.

5. Mazungumzo mafupi kuhus kama kweli Biblia ni neno la Mungu.

a. Ikiwa Biblia inavyovitu ambavyo visingeliweza kuwapo kama mwanadamu ndiye aliyeiandika, basi Biblia ni neno la Mungu.

b. Biblia inavyovitu ambavyo visingelikuwapo kama mwanadamu ndiye aliyeiandika.

c. Zingatia vitu vile vilivyomo katika biblia:

1. Madai kwamba imevuviwa na Mungu.

2. Unabii na Utimilifu wake.

3. Umoja

4. Kutoweza kuharibiwa kwake.

5. Usahihi wa kihistoria.

6. Usahihi wa kisayansi.

d. Biblia haiwezi kukosa kama ilivyothibitishwa katika njia tatu:

1. Mungu hawezi kusema uongo.

a. Tito 1:2

b. Waebrania 6:18.

2. Yesu alithibitisha jambo hili:

a. Kuamua kama watu na matukio katika Agano la Kale ni kweli au hadithi, tunachotakiwa kufanya ni kuona jinsi Yesu aliyekuwa Mwana wa Mungu livyowazungumzia.

1. Aliwataja watu kama Nuhu, Yona, na Adamu kama watu halisi. (Mt.24:37-38, Lk.3:36, 17:26-27,Mt. 12:39-41, Lk.11:29-32)

2. Alizungumzia matukio fulani kama matukio halisi.

3. Roho Mtakatifu aliwaongoza.

a. 2Petro 1:20,21.

C. Mtu anapaswa kufahamu kwamba Biblia sehemu ya Agano la Kale ilitolewa Katika lugha ya kiebrania na Agano Jipya katika lugha ya Kiyunani.

1. Maandishi ya asili ndiyo mamlaka ya mwisho, sio tafsiri tulizo nazo.

2. Agano Jipya ya Kiyunani ndiyo Agano Jipya. Vingine vyote ni tafsiri tu.

2. Mungu aliwaongoza wale waliokuwa wakiandika mwandiko wa kwanza lakini sio wale walio nukulu. Hata hivyo leo hii tunalo neno la Mungu likuwa limetunzwa kwa usahihi kwa kusudi lote.

3. Wanafunzi wa Biblia wanahitaji ikiwezekana kujua lugha iliyotumika au kuhakikisha wanatumia tafsiri iliyo bora.

C. Mtu anapaswa kukubali sababu ya kimaandiko kwamba Mungu alitupa Biblia inayofahamika, ili tuiamini, na kuitii, na kwa hiyo Mungu anatuadhibisha kuifahamu.

1. Isaya 1:18

2. Efeso 5:17

3. Yohana 8:31;32

4. Yohana 20:30,31

5. Mathayo 4:4

6. 2Tim. 2:15

7. 2Tim. 3:14-17

8. Luka 1:1-4

9. Rumi 15:4

10. Wakolosai 3:16

11. Wakolosai 4:12,16

12. 2Thessalonike 3:14

13. 1Thessalonike 5:27

14. 1Wakorintho 14:37

15. Ufunuo 1:1-3

16. 1Thessalonike 5:21

17. Yohana 12:47-50

18. 1Korithiani 1:10-18

19. 1Yohana 4:1

20. 1Timotheo 4:13

21. Efeso 4:14,15

22. Mdo. 17:11,12

23. Mdo. 13:44-46

24. Luka 8:15

25. Efeso 4:1-6

26. Yohana 17:20-23

27. Wafilipi. 1:27

28. Zaburi 1:1-3

D. Mtu anapaswa kutambua kwamba Maandiko matakatifu hufahamika ukiwa na usikivu wa kiroho sawa na wa akili na elimu.

1. Mithali 1:7
2. Tunapaswa kuwa waungwana kiroho vyakutosha ili kuweza kupokea neno la Mungu na uelekevu wa moyo, tukichunguza maandiko matakatifu kila siku kama ndivyo yalivyo. (Matendo 17:11,12)

2. Tunapaswa kujinyenyekeza kama “watoto wachanga” tunaposikia na kujifunza neno la Mungu, kama sivyo, Mungu atatuficha ukweli wake.(Mathayo 11:25,26; 13:10ff; 18:1-4)

4. Tunapaswa kujiangalia jinsi tusikiavyo neno la Mungu; na kuwa moyo mwaminifu na mzuri ambamo mbengu ya kiroho itapandwa ndani yake. (Luka 8:9-18)

5. Mbele za Mungu tunapaswa kuwa “ wa kweli” wanaotawaliwa na “Roho ya Ukweli” (Yohana 18:37; 1Yohana 4:5,6; Yohana 8:46,47)

6. Tunapaswa kuwa na njaa na kui ya neno la Mungu na kupenda kufanya mapenzi yake ili kuweza kufahamu ukweli wa Mungu kwa kuokoa roho zetu (Mathayo 5:6; Yohana 7:17 angalia tafsiri ya Kiyunani ya Yohana 7:17 "akitamaani"

7. Tunapaswa kujitahidi "kutumia kwa halali" neno la Mungu "kukata kati" neno ili tuweze kumpendeza. (2Tim.2:15)

8. Tunapaswa kuwa na imani isiozuilika na chochote katika neno la Mungu ili tumruhusu Mungu awe mkweli lakini kila mwanadamu awe mwongo. (Rumi 3:4)

9. Tunapaswa kukumbuka kwamba katika neno la Mungu kuna vitu, sawa na wanavyopotoa maandiko mengine. (2Petro 3:16-17)

10. Tunapaswa kukumbuka kwamba, "laana" ya Mungu ni juu wale wanaolipotosha neno la Mungu. (Wagalatia 1:6-10).

11. Tunapaswa kujihadhari na wale wanao "haribu neno la Mungu" wanaolitumia neno la Mungu wa udanganyifu. (2Kor. 2:17;4:2-4)

12. Tunapaswa kuwa "wapenzi wakuu wa ukweli" wa Mungu, Mungu asije akatutumia nguvu za upotevu (kuanza kutenda makosa) na kuamini uongo (2Thess. 2:8-12; 1 Wafalme 22:8-23).

13. Tusimwendee Mungu tukiwa na "sanamu" ndani ya mioyo zetu au "kikwazo cha uovu" mbele zetu tusije tuka "jidanganya" (Ezekieli 14:1-11; 33:30-33)

14. Tunapaswa kuachana na "masikio ya utafiti" kiroho ili tuweze kudumu katika mafundisho yenye uzima na kuachana na "hadithi" (2Tim. 4:1-4).

15. Tunapaswa kufahamu kwamba neno la Mungu ni chombo cha kiroho chenye makali kilicho na uwezo wa kukata ndani ya roho zetu, "jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo." (Waebrania 4:12,13)

E. Mtu anapaswa kutafakari juu ya neno la Mungu usiku na mchana.

1. Utangulizi.

   a. Watu wengine hawawezi kugundua ukweli uliojificha unaopatika katika Biblia kwa sababu hawajifunza kujifunza kwa undani; na kumbe ili kupata lulu hii iliyojificha, mtu anapaswa kuendea maandiko matakatifu akiwa nia nzuri ya kiroho na bidii ya kuchunguza hazina iliyofichika.

      1. Ayubu 23:12
      2. Mathayo 4:4

   b. Kwa nini watu wanakosa kupata hazina iliyojificha hii?
      1. Upofu wa kiroho

         a. Yeremia 10:23
         b. Mathayo 6:19-23
         c. Mithali 16:25

2. Uwiano Makosa:

a. Wengine hawatambui uhalisi wa hazina ya maandiko matakatifu iliyofichika kwa sababu wanatumia mizani ya kimwili kutafuta uwiano wa “baraka za kiroho.”

b. Kama tungelipima hazina hii katika mizani ya Mungu, au kuipima kwa kanuni Yake, tungelikuta kwamba ina thamani kuliko fedha au rubia au dhahabu au vito vyenye thamani.
   1. Mithali 16:16
   2. Mithali 3:15
   3. Mithali 20:15

c. Wengine ni mfano ya yule mtu aliyekusudia kubomoa ghala zake ili kujenga kubwa, hawajali kupima thamani ya vitu vya kimwili na thamani ya roho zao (Luke 12:15-21).
   1. Yesu alisema, “Jilindeni na choyo, maana uzima wa mtu haumo katika wingi wa vitu vyake alivyo navyo.” (12:15)
   2. Tena anatuhadharisha kuhusu kujiwekea hazina zetu hapa duniani, badala ya kuwa tajiri kwa Mungu. (12:21)
      a. “Kwa kuwa itamfaidia mtu nini kupata ulimwengu wote akipata hasara ya nafsi yake?” Au mtu a toe nini badala ya nafsi yake? (Marko 8:37)

3. Umadhehebu:

a. Jambo linalowafanya watu wengi wasijishughulishe na kutafuta maandiko matakatifu, wanafikiri hayawezi kufahamika.

b. Wengine wanafikia kukataa tamaa kwa kusema, kwanza, tuna madhehebu karibu miatano nchini basi Ukristo haufanyi kazi.

c. Tukiwa na kutokuelewana kwa namna hii, walio wengi katika madhehebu wamefikia kuamua kwamba,Biblia haifahamiki kwa hiyo hawataki hata kujaribu kuchunguza.
   1. Efeso 5:17
   2. 1Kor. 1:10

4. Kukosa bidii:

a. Ukiamini kwamba ramani ulionayo mkononi ina sehemu zilizofichwa zenye hazina yenye thamani, ungelifanya nini?
   1. Ungeliiacha ikae kwenye kabati?
   2. Ungelisema hii haifai?
   3. Au ungelifanya uwezalo kuifahamu kwa kusudi la kupata hazina iliyofichika?

b. Watu wanakosa bidii ya kupata hazina hii yenye vito vya thamani.

2. Kwa nini hazina hii imefichwa?

a. Hazina hii imefichwa kwa kusudi.

1. Bwana anatafuta walio na njaa na kiu ya neno lake. (Mathayo 5:6), na kwa sababu sisi ni viumbe vyenye hiari ya kuchagua, anataka tuchague kumfuata kwa bidii na kwa upendo.

2. Imefichwa ili watu wasio watakatifu na wasio na busara wasije walichezea na kuligeuza kitu cha kawaida.

a.. Mathayo 11:25
b. 2Kor.4:3-4

3. Wanafunzi walipomuliza Yesu "Kwa nini unasema nao katika mifano aliwajibu:

a. Mathayo 13:10-17

b. Mathayo 13:44

3. Kugundua Hazina iliyofichika:

a. Kugundua hazina hii iliyofichika ndiyo kusudi la mafunzo haya.

1. Inagharimu sana kufahamu kitu.

2. Siku hizi kuna vitu vingi vya papo hapo. Kwa hivyo watu huwa wavivu sana kutafuta vitu vya muda mrefu.

3. Lakini kugundua hazina ya Biblia iliyofichika ni kazi ya milele. Inachukua muda na nguvu nyingi kuipata hii hazina.

b. Hapa tunao ufunguo:

1. Zaburi 1:1-3

2. 119:97-104

a. Huwa mwerevu kuliko maadui zake.
b. Huwa na maarifa hata kuliko walimu wake wote.
c. Huwa na maarifa kuliko wazee.
d. Huondoa miguu yake kila aiana ya dhambi.
e. Hujifunza kuchukia kila njia ya uongo.

3. Yoshua 1:8
3. Warumi 12: 1-2
4. Wakolosai 2:3
5. Wakolosai 3:2
6. 1Tim. 4:15
7. 2Tim. 2:7

8. Wafilipi 4:8
9. Isaya 26:3
10. 2 Nyakati 26:5 kadri Zekaria alivyo mtafuta Yehova "Mungu alimpa mafanikio"

c. Mtu anapoamua kujitunzia hazina yake mbinguni,(Mathayo 6:20) Jicho lake huwa na kusudi moja na mwili wake mzima huwa umejaa na nuru. (6:22)

1. Maana yake ni kwamba unao ufahamu wa kiroho ambao ni kamili.

2. Lakini ukiwa unatafuta hazina ya muda mfupi ya dunia hii, macho yako ni maovu na mwili wako mzima umejaa na giza wewe ni kipofu (6:33)
3. Faida nyingine inayopatikana kutokana na kutafuta hazina ya Biblia iliyofichika, ni mwanga wa kiroho.

4. Unapaswa kufahamu kwamba 2Pt. 20-21 kwa kweli haifundishi
5. kwamba mtu peke yake hawezi kutafsiri maandiko matakatifu.

F. Mtu anapaswa kufahamu kwamba ni lazima kupata kusudi lote la Mungu kuhusu kila somo ili kuweza kupata mapenzi ya Mungu kamili,sehemu ya ukweli hautoshi.

1. Paulo hakuwa na hatia na damu ya watu wote kwa sababu alifudisha "kusudi lote la Mungu" (Mdo.20:26,27)

2. Paulo alifahamu kwamba mara nyingi watu hupenda kupokea nusu ukweli, lakini hawapendi kupokea kweli yote, kwa sababu baadhi ya huo ukweli huwatia hatiani kufuatana dhambi wanazofanya.

3. Utaratibu huo tunauona katika habari za kujaribiwa kwa Yesu na Shetani, Mathayo 4:1-11. Baada ya Yesu kumwelezea Shetani kwamba imeandikwa, Shetani naye alianza kutumia maandiko akisema imeandikwa. Yesu tena akamjibu imeandikwa kwa kuonyesha kwamba Shetani alikuwa akipotosha maandiko matakatifu kwa kumaanisha kile ambacho halikuwa kusudi la Mungu ambalo lilikuwa likitofautiana na maandiko mengine matakatifu katika sehemu zingine za Biblia. Hapa Yesu alionyesha kwamba ilihitaji kusudi lote la Mungu ili kutafsiri vema fungu la maandiko alilolitoa Shetani.

4. Sikuleta fungu la maandiko linalopingana na fungu lingine bali ni kuleta fungu la maandiko linalo funua lingine.

5. Katika mahakama zetu kwa kawaida watu wale wanaotoa ushahidi wanatakiwa kutoa ukweli na ukweli peke yake.

6. Sikutoa "ukweli" tu, bali "ukweli wote" sikitu kingine bali ukweli. Hii ndiyo njia ya pekee ya kuufanya ukweli.
7. Kama watu wangelikuwa wanatumia maandiko matakatifu kama vile wanavyo fuata utaratibu wa mahakama, kusingelikuwa na makosa ya dini, mengi kama tuliyo nayo siku hizi.

8. Makosa ya watu walio wengi katika dini ni kuchukuwa mistari wanayoipendelea huku wakiacha vifungu vya maandiko vinaohusiana na somo husika, na

kupeleka mistari hiyo kiasi kwamba zinapingana na vifungu vingine katika Biblia.

9. Kwa mfano Mathayo 7:1 hunukuliwa sana na waliowengi siku hizi ("Usihukumu usije ukahukumiwa") na kutafsiria kwamba mtu hana haki ya kukosoa, hukumu, au kuweka wazi dhambi au kosa kwa vyovyote. Lakini hawafahamu kwamba Yohana 7:24 Yesu alisema, "Basi msihukumu hukumu ya macho tu, bali ifanyeni hukumu iliyo ya haki." Tena katika 1 Korintho Sura ya tano na Sura ya sita 6: 1-4 mtume aliwaamuru kanisa la Wakorintho kuhukumu. Kwa hiyo ni makosa kutumia neno la Mungu kwa njia mbaya kwa kusema Mungu anawaagiza watu wasihukumu.

10. Funguo tatu za kufungua tafsiri ya Biblia: Thomas B. Warren anaelezea kwamba, ni kukusanya jumla ya ushahidi, kushikilia ushahidi, ndipo kufikia hatimisho..

    a. Jumla ya ushahidi ni kile kinacho saidia hatimisho iliyofikiwa.
        1. Inahusisha yote inayozungumziwa katika neno la Mungu kuhusiana na somo husika.
        2. Bila shaka hili linahitaji bidii ikiwa na maana kwamba unapaswa kuwa na ufahamu wakutosha kuhusiana na Biblia.
        3. Kwa mfano kusudi zima la Biblia linapaswa kufahamika.
            a., Biblia:
                1. Vitabu 66
                2. Agano la kale 39 (Torati, Mashairi, Manabii)
                3. Agano Jipya 27 (Maisha ya Kristo, Historia, Nyaraka, Unabii.)
    b. Roy Deaver anahatimisha kusudi la Biblia kama: "Utukufu wa Mungu, na Wokovu wa mwanadamu, kwa njia ya Yesu Kristo Bwana wetu"
    c. Wayne Jackson: Hakuna mafunzo yenye mchanganuo wa maandiko matakatifu, wenye faida, mwanafunzi wa Biblia anayoweza bila kuelewa kusudi la kitabu hiki cha Mungu. Biblia ni kitabu cha Msingi chenye WOKOVU. Historia , Jiografia , habari kuhusu maisha ya watu , Theolojia, n.k, vinapaswa kutamwa kwa mtazamo huu."

1. Vipindi vya Historia ya Biblia:

    1. Kitabu cha maandiko matakatifu kinapaswa kufahamika kwa kuzingatia kipindi kipindi husika.

    2. Mojawapo ya sababu watu wengi huona biblia kuwa ngumu kusoma ni kwa sababu hawana ufahamu kuhusiana na vipindi kumi na tano vya Historia ya Biblia.

        a. Ukiwa na muhutasari mzuri unaweza kutambua tukio katika historia kwa kipindi fulani.
        b. Bila kuwa na ufahamu wa muundo wa elimu ya miaka na mambo yafuatanayo, ya historia ya Biblia, majina na matukio hufanyika kuwa giza na maelekeano muhimu hupotea.
    3. Uchunguzi ufuatayo utakuwa wa msaada kwako katika kujifunza maandiko matakatifu:
        a. **Kabla ya Gharika (Anteduluvian):** Kutoka kuumbwa hadi gharika. Tarehe zinazowezekana ni 4173 hadi 2517 K.K. Wahusika wakuu: Adamu, Hawa, Kaini, Enoki, Nuhu, (Mwanzo 1-6)

        b. **Baada ya Gharika (Postdiluvian):** Kutoka gharika hadi kuitwa kwa Ibrahimu. Tarehe z inazowezekana ni 2517 hadi 2092 B.C. Wahusika wakuu : Nuhu,

Shemu, Hamu, Japhethi, Nahori,Tera, Lutu, Abramu(Ibrahimu) (Mwanzo 6-11)

c. **Yamababu:** Kutoka kuitwa kwa Ibrahimu hadi kwenda Misri. Tarehe zinazowekana ni 2092 hadi 1877 K.K. Wahusika wakuu: Abramu(Ibrahimu), Isaka, Yakobo(Israeli),Yusufu, Raheli, Leya, Labani, (Mwanzo 12-45)

c. **Utumwa wa Misri:** Kutoka wakati wa kwenda Misri hadi safari ya kuondoka Misri. Takribani tarehe ya 1877 hadi 1447 K.K. Wahusika wakuu ni: Yusufu, Moses, Faraho(Mwanzo 42- Kutoka 11)

d. **Mazunguko:** Kutoka kuondoka hadi kuvuka mto Jordani. Ni takribani kuanzia tarehe 1447- 1407 Wahusika wakuu : Musa, Haruni, Miriamu (Kutoka 12 hadi Kumbukumbu 34)

e. **Ushindi:** Kutoka mto Jordani hadi kuweka Waamuzi. 1407 hadi 1350 K.K. Wahusika wakuu: Yoshua. 1-24

f. **Waamuzi:** Kutoka kusimikwa kwa Wafalme hadi kuanzishwa kwa Ufalme. 1350-1051 K.K. Wahusika wakuu: Samsoni, Ruthu, Naomi, Samweli (Waamuzi 1 hadi 1Samweli 8)

g. **Ufalme:** Kutoka kuanzishwa kwa ufalme hadi kugawanyika kwa ufalme. 1051- 931 K.K. Wahusika wakuu: (Samweli, Sauli, Daudi, Jonathani Solomoni (1Samweli 9 hadi 1Wafalme 11 na 1 Nyakati 10-32)

h. **Ufalme uliyogawanyika:** Kutoka kugawanyika kwa Ufalme hadi kuanguka kwa Samaria. 931 hadi 722 K.K. wahusika wakuu: Eliya Ahabu, Yezebeli, Yeroboam, Elisha, Yehu, (1Wafalme 12 hadi 2Wafalme 20 na 2 Nyakati 10-32)

i. **Yuda Peke yake:** Kutoka kuanguka kwa Samaria hadi kuanguka kwa Yerusalemu. 722 hadi 586 K.K. Wahusika wakuu: Isaya, Hezekia, Yosia (2Wafalme 21-24 na 2 Nyakati 33-36).

j. **Uhamisho wa Babeli:** Kutoka kuanguka kwa Yerusalemu hadi kuanguka kwa Babeli. 586 hadi 536 K.K. Wahusika wakuu : Ezekieli, Danieli, Nebukadreza (2Wafalme 25:8-21 na Danieli 1-8)

k. **Kurudisha:** Kutoka kuanguka kwa Babeli hadi mwisho wa Kanoni ya Agano la
Kale. 536 hadi 500 K.K. wahusika wakuu: Zerubabeli, Esta, Ezra, Nehemia. Vitabu vilivyomo katika Biblia vyenye kuhusika na kipindi cha muda huu ni: Ezra, Nehemia, Hagai, Zekaria, Esta, Danieli.

l. **Kipindi cha Katikati ya Maagano**: Kipindi katika ya Agano la Kale na Agano Jipya. Kipindi cha ukimia wa unabii.

m. **Maisha ya Kristo:** Kutoka kuzaliwa kwa Kristo hadi kupaa kwake mbinguni. Mhusika wakuu: Yesu (Mathayo, Marko, Luka, Yohana)

n. **Kanisa:** Kutoka kupaa kwa Yesu mbinguni hadi mwisho wa Agano Jipya. 33 B.K. hadi leo hii. (Matendo ya Mitume hadi Ufunuo)

b. Kushikilia ukweli huo:
   1) Fikia hatimisho tu kulingana na ushihidi uliyopo.
      i. Usiseme zaidi ya kile kinachotakiwa.
      ii. Usiseme kilicho pungufu ya kile kinachotakiwa.

c. Hatimisho:

1) Ikiwa utaratibu wa kimsingi tuliyo shughulika nao katika somo hili utafuatwa,, hatimisho itayofikiwa hasa hatimisho Mungu angelipenda tufikie, sio zaidi sio pungufu.

F. Mtu anapaswa kutumia mazingira ipasavyo katika fungu la maneno yo yote katika maandiko matakatifu.

1. "Mazingira" maana yake, 1. Sehemu ya sentensi, fungu la maandiko, mazungumzo n.k. inayotokea mara kabla na baada ya neno, fungu la maandiko maalum husika linaloamua maana yake kamili….(2) Jumla ya hali, usuli, au mtu au mambo muhimu yalikuwa yakitendeka kwa wakati huo.

2. Kujifunzi au kufahamu maneno katika mazingira yake ya sasa hivi ndiyo utaratibu unaofahamika na walio wengi ulimwengu mzima. Akili za mtu za kawaida humfanya mtu kuchukulia anachokisikia au kukisoma katika mazingira ya somo, mazungumzo na hali husika.

3. Kwa wakati huo huo, watu waliowengi hajajifunza kujifunza maandiko matakatifu katika mazingira na hali yake au wanaovuta maandiko kutoka mazingira yake na kufanya ielezei mambo amboyo hayamo katika maandiko na kufundisha cho chote wanachokitaka wao. Hili ni kosa la kuasi akili za kawaida na ni dhambi ya kupotosha neno la Mungu, lakini ajabu ni kwamba, wa dini mbali mbali hufanya hivyo. I Tim. 2:9 ff.

4. Moja wapo ya hitilafu ambazo ni hatari ni kutenganisha kwa maandiko matakatifu katika paragrafu. Hili hutenganisha umoja na mazingira na somo, mazungumzo, na matukio, na imesababisha watu wengi kukosa munganisho wa msitari unaofanana.

5. Pia kuna mazingira mapana kuhusu fafanusi zima ya matukio yaliyo panuka kwa mfano (Yohana 13, 14.,15, 16,17, sura) au kitabu kizima kwa mfano mhubiri katika hali yake ya kipekee, vitabu kama Wagalatia, na Warumi- kwa kusema kweli, karibu kila kitabu kinayo mambo ya usuli yaliyo muhimu kufahamu na kukumbuka. Mtu anapotafakari maana ya maneno katika kitabu. Kwa mfano: Imekubaliwa kwamba, uzushi wa Wagnostiki ulikuwa ndiyo sababu iliyomfanya Yohana kuandika waraka 1,2,3 kwa maneno yanayo fanana na hayo, tunayapata katika kitabu cha Wakolosai, na Injili ya Yohana.

6. Tena kuna mazingira ya Biblia zima, umoja wa maandiko matakatifu yote, Uwiano wake wote unaopaswa kukumbukwa. Katika ufasiri na ufafanusi wa maandiko matakatifu hakuna kufunua wazi fungu la maandiko unaloweza kufanya sawa sawa likiwa likipingana na maandiko mengine hata likiwa limeondolewa kwenye mazingira ya karibu.

7. Lakini wakati mwingine mangira ya maandiko matakatifu hutumika vibaya kwa kupunguza au kuongeza matumizi yake. Tunapaswa kujifunza kila mazingira kwa uangalifu kwa kutofautisha vitu vilivyo kuwa vya muda mfupi na vilivyokuwa vya kudumu, yaliyokuwa yakutokea tu, na yaliyokuwa ya lazima, na yaliyokuwa ya utamaduni wa wanadamu wa kipindi husika. Na ikiwapo yoyote inayotofautiana na amri ya Mungu ya kudumu. Daima utaratibu kama huu si rahisi na ndiyo sehemu ngumu ya Hermaniutiks na eksejesis. (1Kor. 13:8ff)

8. Kwa mfano Paulo alisema, wanawake wanyamaze kanisani (1Kor. 14:33-35).

Hapa mazingira ya karibu yalihusu matumizi ya vipawa vya unabii na kunena katika lugha. Wengine wamedai kwamba, kwa sababu vipawa vya unabii na kunena kwa lugha kumekoma, kwa hiyo amri ya kuwakataza wanawake kunyamaza kanisani nayo imekoma. Ni kweli vipawa vya unabii na kunena katika lugha vimekoma, lakini hii haitoi ruhusa kwa wanawake kunena kanisani kwa sababu kuna maandiko matakatifu mengine kuhusu amri hii. (Itim. 2:8-15, Ikor. 11:2-16; Mwanzo 3:16, Waefeso 5:22-23). Kwa hiyo 1Kor.14:33-35 nayo inahusishwa sawa sawa na mistari mingine ya Biblia iliyotajwa.

9. Kuna vitu vya muda na vya kudumu. Kwa mfano Warumi 16:16. Hapa Paulo hatoi utaratibu mpya wa salamu, bali anatumia salamu ambazo walikuwa wakitumia kwa kawaida siku hizo. Leo hii tukisalimiana kwa kushikana mikono tunatumia tabia ambayo ni ya kawaida. Inatakiwa, tunaposalimiana kwa kushikana mikono iwe mikono mitakatifu. Kwa hiyo, tunapaswa kujifunza katika mazingira ya karibu, mapana, makamilifu, tukitenganisha yaliyokuwa ya muda na yale yaliyokuwa yakudumu.

10. Pointi za nyongeza zakutusaidia zilizo muhimu katika kujifunza:
    1. Viwango vinne katika kujifunza:
        a. Kiwango cha mwanzo
        b. Kiwango cha kukagua
        c. Kiwango cha kuchanganua
        d. Kiwango cha kitopiko(somo)
    2. Kanuni saba ya kusoma kwa mchanganuo:
        a. Ainisha kitabu kufuatana na aina ya somo husika.
        b. Elezea kinachozungumziwa halisi katika kitabu ufupi.
        c. Hesabu sehemu zake muhimu kwa mpangilio na uhusiano na kuandika habari kidogo kuhusiana na sehemu hizi.
        d. Fafanua tatizo au matatizo mwandishi alikuwa akijaribu kutatua.
        e. Kuwa pamoja na mwandishi.
        f. Fahamu hoja ya mwandishi.
        g. Shika insha ya mwandishi.

11. Maelezo kamili kuhusu kanuni zenye mchanganuo saba hizi:
    a. Kanuni ya uchanganuzi #1- Ainisha kitabu kulingana na hali na somo husika.

        (1) Masimulizi:

            (a) Biblia imebeba masimulizi mengi sana kuliko kitabu chochote.

                1. Kupita 40% ya Agano la Kale ni masimulizi.

                2. Vitabu hivi vimezidi masimulizi: Mwanzo,

                Yoshua, Waamuzi, Ruth, 1&2 Samweli, 1&2 Wafalme, 1&2 Nyakati, Ezra, Nehemia, Danieli, Yeremia, Hagai, Mathayo, Marko, Luka, Yohana, na Matendo ya Mitume.

            (b) Masimulizi ni hadithi za kweli.

                1. Kusudi la masimulizi hayo imezidi na

mafundisho; hiyo ina maana kwamba, imeandikwa kwa kusudi la kufundisha ukweli wa kiroho mkuu.

2. Kwa sababu hii, Wakristo wa leo wanapaswa kujifunza Agano la Kale.
   a. Warumi 15:4; 1Kor. 10:11
   b. Bila kujifunza Agano la Kale, mwanafunzi wa biblia atakuwa bila msaada katika kufahamu sehemu kubwa inayofundishwa katika Agano Jipya.
3. Ingawa hakuna kitu chakutufunga, lakini tunafungwa na kusudi la kimsingi.

(c) Kile ambacho si masimulizi:
1. Masimulizi ya Agano la Kale si hadithi tu kuhusu watu walioishi kipindi cha kale.
   a. Ni habari kuhusu kile Mungu alichowafanyia watu hao au alichokifanya kupitia wao
2. Masimulizi haya si maneno yaliyojaa hekaya za kubuni.
   a. Masilimuzi hizi hazijibu maswali yote kuhusu kila swali kwa hiyo hatu stahili kuelezea jinsi tupenda-vyo katika kuelezea maana yake.

2.Sheria:

(a). Agano la Kale lina zaidi ya sheria 600 walizopewa wana wa Israeli walizotakiwa kutunza kama ushahida wa kumtii Mungu.
1. Vitabu vinne katika Agano la kale vina sheria. Hivyo ni Kutoka, hadi Kumbukumbu. Kitabu cha Mwanzo nacho hiitwa kitabu cha sheria kimsingi. Hizi ni sheria walizopewa mababu kuanzia Adamu hadi Yusufu.
2. Wakati mwingine waandishi wa Agano Jipya huita Agano la kale lote kama sheria.(Mathayo 5:17-18; Luka 16:17

3.Manabii:

(a) Vitabu vingi katika Biblia vinapatikana katika kichwa hiki kuliko kingine.
1. Manabii wakuu wanne(Yeremia, Isaya, Ezekieli na Danieli).
2. Manabi wa dogo 12
   1. Wanaitwa manabii wadogo kwa sababu maandishi yao ni mafupi.

(b). Manabii walisaidia watu kuheshimu Agano la Kale.
1. Mungu hakutoa sheria yake tu bali alitaka watu watii.
   a. Alitaka watu watii kwa kuwapa baraka wanaotii.
   b. Alitaka watu watii kwa kuwapa laana wale wasiotii.
2. Hapo sasa ndipo manabii waliingilia kati.
   a. Mungu alitangaza baraka kwa wanaotii na laana kwa wasiotii kupitia manabii.(Kumbukumbu 28-32)
   b. Laana walioitangaza kwa wasiotii hawakuwa na uwezo wa k uibadilisha. Walikuwa wakilitoa neno la Mungu kwa kuvuviwa.
   c. Tunaposoma manabii, tunasoma sheria ya Musa ikiwekwa katika vitendo katika kipindi husika.

(d).Kazi ya mosomaji wa siku za leo ni kujenga upya vizuri iwezekanavyo kadhia ya kihistoria iliyo wazunguka manabii utakao kuwa ukisomo leo hii.

1. Nabii huyu anaingia wapi katika orodha ya matukio katika kipindi husika?
2. Nabii huyu alikuwa nani?
3. Aliwaandikia wanani?
4. Ujumbe wake ulilenga nini? Ni kadhia zipi zilizomfanya aandike?

(4).Mithali(mifano): Fananisha

a. Mifano ni kitu kilicho sahihi katika maisha, kikifananishwa kuleta maana ya kiroho.
b. Sababu nne ya mithali au mifano:
    1. Kufanya ukweli wa kiroho wazi kwa wale wanaoutafuta kwa uaminifu mapenzi ya Mungu.
    2. Kuwaficha ukweli wasio waaminifu.
    3. Kuwafanya watu kuona ukweli kabla hawajaona kwamba unawahusu wao.
    4. Kuwasaidia watu kukumbuka ukweli (mfano wa Msamaria mwema, Mwana mpetevu)

(5).Nyaraka:

(a). Kwa jumla, nyaraka z a Agano Jipya zilifuata namna fulani:

1. Jina la mwandishi
2. Jina la waandikiwa.
3. Salamu
4. Sala na shukurani.
5. Mwili (mazungumzo)
6. Salamu za mwisho na kuagana.
    a.Hakuna sala katika kitabu cha Wagalatia, 1Timotheo, Tito.
    b.Shukurani na wimbo wa kumsifu Mungu ni katika 2Koritho, Efeso, 1Petro, na Ufunuo.
    c.Waebrania haina mambo hayo matatu tuliyo yataja hapo juu.
    d.Yakobo na 2Petro haina salamu na kuaga kunaofanana.

(b). Nyaraka za Agano Jipya ziliandikwa kukidhi mahitaji fulani.

1. <u>Waraka kwa Warumi</u> uliandikwa kuwashawisha Wayahudi kwamba, injili ndiyo kweli ya ukamilifu wa sheria na manabii uliotabiriwa, na kuonyesha hitaji la mwanadamu la kupata ukombozi na namna ya kuupata .
2. <u>1Wakorintho</u> ilikusudia kurekebisha roho wa mafarakano katika Korintho na kujibu maswali waliokuwa wamemtumia Paulo.
3. <u>2Wakorintho</u> zaidi inazungumzia namna Paulo alivyokuwa akiutetea utume wake.
4. <u>Wagalatia</u>. Ilikusudia kurekebisha fundisho la uongo walilolifundisha wadugu waliotoka katika dini ya Wayahudi waliotaka kuwalazimisha wakristo kushika sheria ya Musa na kutahiriwa.
5. <u>Efeso</u>. Waraka huu, unalenga kanisa la Kristo.
6. <u>Wafilipi</u>. Ni waraka wa upendo aliowaandika Paulo akiliandikia kanisa lilomsaidia katika kazi yake.
7. <u>Wakolosai</u> waraka huu unalenga Kristo na kanisa lake na ukuu wake Kristo.
8. <u>1Wathesalonike.</u> Waraka huu unatatua kutokuelewa kwa wadugu waliokuwa nao kuhusu kurudi kwa Yesu mara ya pili.
9. <u>2Wathesalonike</u> Waraka huu nao unarekebisha. Paulo anawasihi wandugu kuachana na uvumi.
10. <u>1Timotheo</u> waraka huu ulikusudiwa kumsihi Timotheo kupigana vita vizuri (6:12)
11. <u>2Timotheo</u> waraka huu ulikusudia kumtia nguvu Timotheo asitayarike. 2Tim. Huhatimisha waraka: “Bali wewe uwe na kiasi katika mambo yote, vumilia mabaya, fanya kazi ya mhubiri wa injili, timiliza huduma yako.

12. Tito Ni waraka wa Paulo kwa Tito akimkumbusha kwamba atengeneze mapungufu katika kanisa, kwa kuwachagua waz ee wa kanisa. (1:5)
13. Filemoni. Ni waraka uliojaa upendo kutoka kwa Paulo ukimwendea Filemoni ili ampokee mtumishi wake Onesimas aliyekuwa amemtoroka.
14. Waebrania. Ni waraka wenye k usihi na kuhojiana na wale waliokuwa tayari kurudia dini yao ya kiyahudi akiwaonyesha kwamba Kristo na u kristo ulikuwa mkuu kuliko kuliko agano la kale na dini ya kiyahudi.
15. Yakobo ni waraka uliokusudia kuelezea maisha ya mkristo katika vitendo. Unaelezea dini ya kweli isio na taka mbele za Mungu ni ipi.
16. 1Petro. Huu ni waraka wakusaidia kuvumila majaribu yanayotujia.
17. 2.Petro. Waraka huu unalenga ahadi ya Mungu yenye thamani kuu akilinganisha na ahadi bure walizokuwa wakitoa waalimu wa uongo.
18. 1Yohana. Waraka huu unaelezea matatizo ya mpinga Kristo.
19. 2Yahana. Huu ni waraka ulioandikiwa mtu binafsi, ya mama ambaye jina lake halikutajwa mwenye watoto waliokuwa wakienenda vizuri katika kweli.
20. 3Yohana .Waraka huu unazungumzia ndugu wa ushindani aliyependa kuwa mkubwa kanisani. Kama si yeye kutawala ilikuwa kuharibu.
21. Yuda. Waraka huu unakwenda sambamba na yale ya 2Petro 2 kwa hiyo inalenga waalimu wa uongo na kuwaonya wandugu kuhusu nia yao.

(6). Maandishi ya Yasiyokubalika(ya uongo)Apocalyptic Literature:

(a) Maana:

1. Walter Bauer anafasiri neno “apokalupsis” “ufunuo, weka wazi, kile ambacho hakijafunikwa.”

2. Maana inayowezekana kuwa bora ni kwamba ni mfano unaoonyesha picha maangamizi ya waovu wa ulimwengu inayokuja inayoahidi pia ushindi wa wenye haki. Katika maana hii inayokubalika na wengi, kuna sifa kadhaa maalum.

3. Kusudi la mwandishi haikuwa kufunika ujumbe wake bali ni kuufanyaj wazi. Iliandikwa kwa njia ya kuficha ukweli kwa maadui na kuufunua maana yake kwa wateule.

(b) Aina ya:

1. Yenye kanoni na isio na kanoni.
2. Agano la Kale na Agano Jipya.
   a. Agano la Kale
      1. Ezekieli
      2. Daniel
      3. Yoel 1-2
      4. Zechakaria
   b. Agano la Kale:
      (1) Mathayo 24-25; Marko 13; Luka 21
      (2) Mdo. 2:17-21
      (3) Ufunuo.
   c. Sifa ya maandiko ya siri yenye kanoni:
      1. Daima ina maana ya kihistoria

a. Hali fulani ya historia ya kigomvi inahusiana na kuandikwa kwa kitabu.
b. Historia inatazamiwa kama yenye kufunua mpango wa Mungu, na kwa hiyo, matokeo yake hayaepukiki…..hii haikatazi uhuru wa kila mmoja.
b. Inahusiana na eskatolojia(mafunzo ya vitu vya mwisho.)
c. Kwa hiyo ufahamu wa hali ya kihistoria inayohusiana na k itabu ni wamaana kwa kuelezea kwa undani kitabu.
d. Wakati wa tukio kubwa wa kukumbuka.

2. Ujumbe zaidi hutolewa kwa njia ya maono.
   a. Ni jambo la kuangaliwa la kipekee katika aina ya maandiko.
      1. Ufunuo 1:11 “Uyaonayo uyaandike katika chuo….”
      2. Ufunuo 4:1 “Baada ya hayo naliona…..”
3. Kuna aina ya utabiri:
   a. Danieli 2,7, 8.
4. Sifa nyingine ya maandiko ya kiapokalyptik ni matumizi ya alama.
   a. Tarakimu.
   b. Maneno ya kuleta maana akilini.
   b. Mtu anahitaji kufahamu kwamba tafsiri sahihi ya alama hizi mara kwa mara inahitaji ufahamu wa ndani wa kusudi ili isipelekwe badala ya kuongeza maana katika linalozungumziwa.
   c. Ya alama inayohusu ulimwengu:
      1.)Ufunuo 6:12-13; 8:12.
      2.)Isaya 13:6-10
      3.)Isaya 34:4-5
      4.)Ezekieli 32:7-8
      5.)Mathayo 24:29-31
      6.)Yoel 2:1-2,10
      7.)Amosi 8:9
      8.)Haggai 2:6-7,21-22.
      9.)Isaya 19:1
5. Faraja.
6. Ya siri: “Siri za Mungu katika kuingilia kati katika historia ya maisha ya wanadamu imefunuliwa, lakini mara nyingi katika njia ya jumla.

(7) Maandishi ya kimashairi:

(a) Orodha ya Zaburi

1. **Zaburi za maombolezo**: Hizi ni sala zinazoelekezwa moja kwa moja wa Mungu na mtu binafsi au na kundi la watu hasa wakati wa mahangaiko. Kawaida zinahusisha maelezo ya aina ya tatizo, ukiri wa tumaini na kiapo cha sifa kwa Mungu. Kutamka ukiwa na uhakika kwamba Mungu anaweza kuwakomboa watu wake.(Mifano Zaburi 3-7,22,42).

2. **Zaburi za shukurani**: Zaburi hizi hutolewa hadharani na yule au waabudu wengi, wakitambua matendo ya Mungu ya uaminifu kwa niaba ya watu wake katika siku za nyuma, au kuonyesha uhakika wao katika matendo ya siku zijazo. (Mifano 18,27,62).

3. **Zaburi za Sifa:** Nyimbo hizi zinategemea neno "Hallelluya" Ni usemi wenye furaha wa kumsujudu Mungu kwa ajili ya ukuu wake, tumtambua kama muumba, msaidizi na mpenda watu wake. (Mifano 113, 117, 146-150)

4. **Zaburi za kifalme**: Nyimbo zenye kuelezea Mfalme, wa kidunia na wa mbinguni, akitawala ufalme wake: (Mifano 2,95,96).

5. **Zaburi za laana**: Mashairi ya kuelezea uchungu wa haki wa mutunga zaburi kwa maadui wa Mungu akitaka kisasi cha Mungu kitolewe haraka. (Kwa mifano 49,109,137) Pia huitwa Zaburi laanifu.

6. Zaburi zenye Acrostik. Mashairi yenye mtindo wa hali ya juu, ambamo kila sehemu mpya ya msitari, huanza na alfabeti ya Kiebrania.(Zaburi 9, 10, 25, 35,119)

7. Zaburi za kuhiji: Nyimbo waabudu walizokuwa wakiimba wakiwa safarini kwenda Yerusalemu wakati wa sherehe ya mwaka. (Zaburi 120-134) Pia huitwa "nyimbo za mpando."

8. Zaburi za kimasihi: Nyimbo za kiunabii zikielezea kuja kwa Masihi kama Mfalme(Psalms 2,24,110) Mtumwa (Zaburi 22,23,40,69) na Mwana wa Mungu(Zaburi 118).

(b) Usambamba: Mashairi mengi tunasoma vina katika maneno. Waebrania walikuwa na neno vima tusiweza kufurahia katika tafsiri ya kiswahil, lakini pia yalikina mawazo tunayoweza kufurahia. Zaburi hizi zimejaa na mistari miwili inayofanana katika mawazo. Ukweli ni kwamba utakutana na aina tano ya vina vya Kiebrania vinaoitwa Usambamba wa Kiebrania.

1. **<u>Yenye maana moja(Synonymous):</u>** Wazo katika msitari wa kwanza linarudiwa katika msitari wa pili.

    a. Zaburi 19:1
    b. Ukweli mshairi anaotaka kuelezea, unarudiwa kwa kuwekea mkazo.

2. **<u>Ya kilicho kinyume(Antithetic):</u>** Wazo alilolizungumzia katika msitari wa kwanza huwekwa kinyume na msitari wa pili.

    a. Zaburi 1:6

3. Ya kufanyiswa, si ya asili(Synthetic). Msitari wa kwanza na wa pili huwa na uhusiano wa tendo na matokeo….azimio na hitimisho. Huwa ndani ya na usilloji(Syllogism-hoja yenye sehemu tatu. Zaburi 23:1

4. Ihusuyo tabia ya nchi (climatic) Wazo la msitari wa pili hupanua na kutilia nguvu wazo katika msitari wa kwanza. Zaburi 29:1

5. Yenye mfano/mithali(Emblematic): Msitari wa kwanza hutumia neno la picha kuonyesha mfano wa maanza inayoelezewa katika msitari wa kwanza. Zaburi 42:1

C. Neno la picha. Kwa nyongeza kwa usambamba, Zaburi zimejaa na lugha ya mfano nyingi zenye kusudi la kuchora picha akilini mwetu kwa njia ya kuonyesha ya kinyume, kutilia mkazo, kueleza wazi.

1. Mfano wa maneno (Simile): Mulinganisho ulioelezewa kati ya vitu viwili vinao fanana.

   a. Zaburi 1:3
   b. Pia na Zaburi 1:4, 5:12;17:8

2. Mfano wa maneno(Metaphor) Mulinganisho ambao kitu kingine hutangazwa kuwa kitu kingine.
   a. Zabuli 84:11
   b. Pia na 23:1; 91:4
3. Ya kupiga chungu au kuongeza ukuu(Hyperbole): Matumizi ya kuongezea chumvi(kwa kiswahili kinachoeleweka na wengi) kwa kusudi la kuwekea mkazo.
   a. Zaburi 6:6
   b. Pia 78:27;107:26
4. Ya kuhusiana na mwanadamu Uanthropomorfi. (Anthropomorphism): Kuchukua kiungo cha mwanadamu na kukifanya kama kiungo cha Mungu.
   a. Zaburi 31:2
   b. Pia na 11:4,18:15;32:8

5. Kufanyika kuwa kama ni mtu (Personification). Kupatia kitu kisicho na uhai sifa za mwanadamu.

   a. Zaburi 35:10
   b. Ona pia 77:16;96:11; 104:19

b. Kanuni ya kimchanganuo # 2- Elezea kitabu kizima kinahusu nini kwa ufupi.

(1) Tayari tumefanya jambo hili kwa kiwango Fulani katika mazungumzo yetu kuhusu nyaraka.

(a) Pasipo shaka, kila kanuni ya kusoma inapaswa kuwekwa akilini unaposoma kitabu chochote,lakini kitabu kinapaswa kusomwa kwa ukamilifu ili kukubaliana na kila kanuni.

(b) Wayne Jackson katika kitabu chake,(“A Study Guid to Greater Bible Knowledge”) Mwongozo wa kujifunza unaokuelekeza kwenye ufahamu wa Biblia. Anatoa mapendekezo ya fuatayo:

1. Soma kila kitabu cha Biblia mwenyewe, na baadaye kwa ufupi, elezea kusudi kuu la kitabu.

2. Ndipo baadaye utahatimisha kwa kuangalia vitabu vya watu wengine kuona kama mmefikia makadirio sawa.

a. Mkikubaliana utafahamu kwa nini mnakubaliana.

b. Msipokubaliana utafahamu pia kwa nini.

c. Hutaondoka na kusema, unakubaliana au hukubaliani na wanachosema bila kufikiria kuhusu kile walichokisema.

2. Mifano:

(a) Kitabu cha Mwanzo ni kitabu cha mwanzo, mwanzo wa dunia, uhai, ,mwanadamu, dhambi, ukombozi, familia, n.k.

c. Kitabu cha Kutoka sawa na jina lake, kinazungumzia wana wa Israeli kutoka katika utumwa wa Misri. Jambo lingine muhimu ni kwamba, sheria alizopewa Musa nazo hupatikana katika sura ya 20 na zinazofuata.

3. Pamoja na kujipatia mhutasari wa kila kitabu, kujifunza kwako pia kutakusaidia kuweka kiwango juu ya kila maana ya kitabu.

a. Unapaswa kujiuliza jinsi fungu la maandiko unalojifunza linakusaidia kuendeleza kusudi kuu hilo.

d. Kanuni ya kimchanganuo #3- Taja sehemu kuu moja moja kwa utaratibu, na husiano na kuautilaini sehemu hizi jinsi ulivyo autilaini kitabu kizima.

1. Vitabu vingine unaweza kuvigawanya katika njia mbili au zaidi.

2. Kwa mfano Kitabu cha Mwanzo unaweza kukigawanya katika njia tatu.

Unaweza kugawanya kwa kufuata wenye sifa wakuu:

(a) Ibrahimu Sura 1-25

(b) Isaaka Sura21-35

(c) Yakobo Sura25-50

(d) Yusufu Sura 37-50

Unaweza kugawanya katika sehemu mbili:

a. Utangulizi 1-11

b. Mababu 12-50

Ama unaweza kugawanya na maneno yanayoanza kwa kusema, Hivi ni vizazi.

a. Hivi ni vizazi vya mbingu na nchi. 2:4

b. Hiki ni kitabu cha vizazi vya Adamu 5:1
c. Hivi ndivyo vizazi vya Nuhu 6:9

d. Hivi ndivyo vizazi vya wana wa Nuhu (10:1)

e. Hivi ndivyo vizazi vya Tera (11:27)

f. Hivi ndivyo vizazi vya Isaac (25:19)

g. Hivi ndivyo vizazi vya Esau (36:1)

h. Hivi ndivyo vizazi vya Yakobo (37:2)

3. Autilaini ya 1Wakorintho kwa ufupi:

I. Kujali kwa Paulo…….Sura 1-6

A. Mgawanyiko……...….Sura 1

B. Mgawanyiko unayakinishwa……...Sura 2-4

C. Nidhamu inaelezewa……Sura5-6

II. Kujali kwa Kanisa lililokuwa Korintho…..Sura7-16

A. Ndoa……Sura 7

B. Sanamu……..…Sura 8-10

C. Tabia mbaya……...Sura 11

D. Vipawa vya kiroho……Sura 12-14

E. Ufufuo……Sura 15

F. Changizo kwa watakatifu……...Sura 16

d. Kanuni ya kimchanganuo # 4- Elezeo tatizo au matatizo yaliyotatuliwa na mwandishi.

1. Kama tayari tumekwisha ona kwamba vitabu vingi vya Biblia viliandikwa kukabiliana na matatizo Fulani. Baada ya kugundua matatizo katika kila kitabu unachojifunza, zingatia namna mwandishi anavyotatua matatizo yaliyomo.
2. Kwa mfano:
   a. Mwandishi wa kitabu cha Waebrania alikuwa akishughulika na ndugu waliokuwa wakimgeuzia Kristo mgongo na kurudia sheria ya Musa kwa kuogopa mateso.
      1. Anawaonya kwa kuwakumbusha kwanza kwamba Kristo ni mkuu kuliko wale wote waliohusika na Sheria za Agano la Kale.

         a. Ni mkuu kuliko malaika (Sura 1)
         b. Ni mkuu kuliko Musa.(Sura 3)
         c. Ni mkuu kuliko Yoshua(Sura 4)

d. Ni mkuu kuliko Haruni (Sura 5)

2. Anawaonyesha pia mapambanisho kadha yenye kuanza na neno (“bora”) Akionyesha kwamba Agano Jipya ni bora kuliko la Kale. Agano Jipya hutoa:
   a. Tumaini bora (7:20)
   b. Agano bora (7:22)
   c. Huduma bora(8:6)
   d. Ahadi bora (8:6)
   e. Dhabihu bora (8:6)
   f. Milki bora (10:34)
   g. Nchi bora (11:16)
   h. Ufufuo bora (11:35)

3. Waraka huu ulikusudia kusihi (13:22) Pia kuna maonyo mengi. Maonyo haya yanaanza kwa kusema, “na tu…”

   a. 4:1
   b. 4:11
   c. 4:14
   d. 4:16
   e. Pia tujifunze mafungu yanayoanza na neno “na tu…” 6:1; 10:22-24; 12:28; 12:1. 12:28, 13:13;13:15

4. Watakatifu wa karne ya kwanza walikuwa watu wenye sifa za vita, mateso kwao lilikuwa ni jambo la kawaida. Imani yao ilijaribiwa na mateso.
   a. Waebrania 10:32-36

5. Katika hali halisi, anawasihi kwamba litakuwa jambo lisilo la busara kurudia kile ambacho ni hafifu ambacho kinachakaa na karibu na kutoweka(8:13)

(3) Ebu na tutumie kanuni namba nne kuhusu kitabu cha Agano la Kale.

a. Tukumbuke manabii hawakuwa watu wa kutabiri mambo yanayokuja tu, bali walikuwa wakielezea watu maneno kutoka kwa Mungu.

b. Kazi yao ilikuwa si kuleta sheria mpya bali kuwaelezea watu kurudia sheria ya Mungu.

   1. Utawala wa Ashuru ulikuwa ikipata nguvu, karibu na kuwa mashine ya vita.

   2. Tayari maandishi yalikuwa

ukutani kwa sababu ya Israeli.

a. Israeli alikuwa amefanya ukahaba na miungu ya Wakanaani.
b. Kwa makusudi wali-kataa maarifa na kuamua kutokumjua Yehova. (4:6,5:4) kiburi kilipo wapanda, wakamsahau Yehova.13:6)
c. Alikuwa amepanda upepo na kuvuna kimbunga.(8:7)
d. Walijitoa kuabudu Sanamu na kunajisika kama sanamu zenyewe walizozipenda. (9:10)
e. Mungu alituma manabii wake wakiwaambia kutubu, bali wao waliku-wa wameamua kurudi nyuma.(11:7) wakiendelea na uongo wao na ukiwa (12:1)

e.Kanuni ya kimchanganuo #5- Kubaliana na mwandishi kwa kufafanua maneno yake makuu.

1.Namna ya kutafuta maana ya maneno:

a. "…..unapaswa kugundua maana ya neno usilolielewa kwa kutumia maana ya maneno unayoyaelewa katika mazingira ya yale unayoelewa.

1.Maneno yanayozingira lile neno ndiyo mazingira ya lile neno linalofafanuliwa.

b. Mchanganyiko wa hali ya mambo:

1.Maneno mengine yana maana kadha tofauti na yanaweza kutumika katika maana moja ama katika maana iliyounganika.

a.Kwa mfano mauti, (-mekufa) hali ya kufa, Yakobo 2:26; Isaya 59:2; Warumi 6:7

2.Hapo kuna shida ya yenye maana moja,mahali ambapo neno moja limetumika kwa maana tofauti.

3.Hiyo ni hali tofauti ya mafungu ya maandiko,

a. Mafungu ya maandiko mawili yanaweza kuelezea maana moja na pia fungu moja la maandiko linaweza kuelezea maana kadhaa
b. Kwa mfano"Kufia dhambi"na "kufa"(katika Warumi 6)

(2). Faida ya kujifunza maneno:

a.Bw. Richard Chenevix Trench, katika kitabu chake (**On the Study of Words) Kujifunza maneno.** Aliandika hivi:

"Kujifunza maneno itakulipa bora zaidi kuliko unavyoamini. Nina uhakika, kiasi kwamba, kwa kila kijana katika uvumbuzi wake kwamba maneno ni nguvu zilizo hai, ni vazi la kufunika mwili, yenye mawazo yanayojisokota pamoja yenyewe, ambayo yamekuwa kama magamba yanayodondoka kutoka machoni, sawa na kupata akili nyingine, ama kutambulishwa katika ulimwengu mpya; hakomi kushangaa tabia yenye mshangao yanayomzunguka pande zote, yanayojifunua kwake zaidi na zaidi anapoangaza macho." (Ukurasa 9-10)

b.Anaendelea kwa kusema, "Kuna wakati mwingine,ambapo maarifa yenye thamani yanaweza kueleweka kutokana na historia ya ya neno kuliko historia ya kampeini." (Ibd.,p.12)

c.Michael Green katika kitabu chake **Evangelism in the Early Church**, Uinjilisti katika Kanisa la Awali. Anatuhadharisha kwamba, "Ni rahisi sana kudanganywa na neno Fulani katika ***kujinga mnara wakitheolojia*** juu yake ambao haukukusudiwa" (Ukurasa 48)

UKURASA WA UCHUNGUZI

_____

KITABU

KISA (KWA NINI ALIANDIKA):_____

MWANDISHI:_____ TAREHE_____

MISTARI MUHIMU_____

MANENO MUHIMU_____

AUTILAINI(UMBO)

_____
_____

WAZO KUU(KILA SURA)

1._____

2._____

3._____

4._____

5._____

f.Kanuni ya kimchanganyiko # 6 Fahamu kusudi la mwandishi linalo ongoza kwa kushughulikia sentensi zake zilizo muhimu zaidi.

(1) Kanuni 5,6, na 7 huenda pamoja.

(a) Kanuni # 5 tafuta maneno yaliyomuhimu zaidi na kukubaliana nayo.
(b)Kanuni #6 tafuta sentensi zilizo muhimu na kugudua kusudi lililomo.
(c)Kanuni #7 tafuta na kujenga hoja ya msingi katika vitabu ukipata uhusiano wa sentensi.

(2) Tunapataje sentensi muhimu katika kitabu?

(a) "…..moyo wa mazungumzo yake hukaa katika maneno aliosema kwa uthabiti na makanusho anayoyafanya, na sababu anazozitoa kwa kufanya hivyo" (Mortimer Adler, ukurasa 121)

(b) Kidokezo kingine kuhusu sentensi muhimu hupatika katika maneno yanayoiunda hizo sentensi.

1. Ukisha tambua maneno yaliyo muhimu zaidi, yanapaswa kukuongoza kwenye sentensi muhimu.

(c) Sentensi muhimu itakuwa pia sehemu hoja kuu ya kitabu.

1. Inapaswa kuwa matangulizi au hatimisho.

2.Hii inahitaji kuwa mtu wa kutambua kisa unapokiona.

a. Kisa : Kisa huwa na mazimio kadhaa, ambayo mengine yanafanya kama sababu(yaani yafanya kama uthibitisho) na moja au zaidi hufanya kama hatimisho (hii ni kwamba, madai hufanyika kwamba hatimisho ni la kimantiki kufuatana na sababu….." (Thom. B.Warren, logic and the Bible. p. 10)

3.Ni muhimu pia kwamba, kufahamu huwa pamoja na utambulisho unaoelekeza kwenye maazimio.

a. Njia nzuri ya kujaribu ikiwa unafahamu kile kinachothibiti-shwa, au kukanushwa, katika uthibitisho au ukanusho wowote ni kuyaweka katika maneno yako mwenyewe.

1. Ikiwa huwezi kufanya hivyo, ni kuonyesha kwamba hujahamu kinachozungumziwa.

H. Mtu anapaswa kutambua kwamba kuna baadhi ya mambo yaliyokuwa ya muda na ya kudumu katika Biblia yanayowafunga watu wote wa kila kizazi.

1. Wasomi wa Biblia wanatambua kwamba, kutambwa ni nini kilicho kuwa cha muda na kipi kilikuwa cha kudumu ni kazi ngumu.

2. Ya muda ni ile yenye uhusiano wa kimababu Mungu alioushikilia katika kizazi cha awali cha wanadamu. Pia na sheria ya kipindi cha Musa, iliyo chukuwa muda wa miaka elfu kumi na nne ikiwafunga wajuku wa Ibrahimu kwa njia ya Isaka na Yakobo, haimfungi mtu yeyote awe Myahudi au Mtaifa.

3. Wengi wanakubaliana kwamba vipawa vya Roho Mtakatifu walivyo kuwa navyo mitume na watu katika karne ya kwanza, vilikuwa ni vya muda, kwa sababu vilitumika kwa kusudi la muda na muhimu, kuthibitisha neno la Mungu kuwa na la kweli katika ushuhuda wake wote. (Mk.16:15-20; Waebrania 2:1-4)

4. Wengi wanaamini kwamba "busu" katika Warumi 16:16 ilikuwa ya muda na ya hiari.

HERMANUITIKSI II

A. Utangulizi:

1. Ni muhimu, tunapojifunza kitabu chochote cha Biblia kuweza kutofautisha:
   a. Ya kudumu ya ya muda.
   b. Ya kuhusu tamaduni na ya kanuni ya kimsingi
   c. Ya lazima na iliyotokea tu kwa bahati
   d. Ya kawaida(Ya –ote) na ya maalum
   e. Agano la Kale na Jipya
   f. Ya tofauti na ya kutopatana
   g. Ya wazi na ya kumaanisha (isiyofahamika)

B. Ya kudumu na ya muda:
Thomas B. Warren katika mafunzo aliyo yafundisha katika chuo kikuu cha Ukristo cha Abilene (Abilen Christian College Lectures pp. 392- 408) iliyopewa jina "Examples and Patten Authority" (Mifano na Kielelezo cha Mamlaka) aliandika, swali la kujiuliza linatakiwa kupangwa hivi, " Nilini, kitendo katika Agano Jipya kinaweza kuchukuliwa kama mfano wa kufuata kwa watu wa leo?"

Zingatia: Ameandika kitabu kinachojulikana kama, "Ni lini mfano huwa unafunga watu" (When is An Example Binding?) Ambacho kinafaa sana kwa kujibu swali hili.

1. Baadaye anakusanya vitendo kadha katika Agano Jipya katika vikundi vitano:
   a. Vitendo ambavyo vilikuwa vya dhambi kwa watu wa kipindi cha Agano Jipya ambavyo ni dhambi kwa watu waleo.
   b. Vitendo ambavyo vilikuwa vya hiari na vya muda(maana yake ni kwamba vilikuwa vya hiari kwa watu wa kipindi cha Agano Jipya lakini si vya hiari kwa watu waleo.
   c. Vitendo ambavyo vilikuwa vya hiari na vya kudumu (maana yake ni vitendo ambavyo vilikuwa vya hiari kwa watu wa kipindi cha Agano Jipya na bado hiari kwa watu wa leo.)
   d. Vya lazima na vya muda (maana ni, vitendo vilikuwa vya lazima kwa watu wa kipindi cha karne ya kwanza katitka Agano Jipya lakini si vya lazima kwa watu wa leo.)
   e. Vya lazima na vya kudumu. (maana ni kwamba vitendo vilikuwa vya lazima kwa watu wa kipindi cha Agano Jipya katika karne ya kwanza na bado ni vya lazima kwa watu wa kipindi hiki.)
2. Ya kuhusu tamaduni za watu na ya kanuni ya kimsingi
   a. Troy Cummings alielezea kwamba, " Wasomi wa Biblia wengi hukubaliana kwamba, kuamua ya muda ya siyokuwa ya muda wakati mwingine huwa ni vigumu sana."
      i. Lakini yeye Thomas B. Warren bado alikuwa akielezea, "Swali linalotakiwa kufikiriwa linafaa kuelezewa ifuatavyo: 'Ni lini tendo linalo elezewa katika Agano Jipya huchukuliwa kama mfano unaowafunga watu siku hizi?'"

ii. R.C. Sproul katika kitabu chake (Know Scripture) Yafahamu Maandiko Matakatifu anapendekeza kwamba, namna tamaduni zinavyo ingia katika maandiko matakatifu ni: Kwa kiasi gani Biblia inavyo husiana na mamlaka yenye mipaka kutokana na miundo na jinsi vitu vionekanavyo kwa macho katika vifungu vya Biblia.

iii. Wayne Jackson, naye anasema, "Isipokuwa mtu akiamini kwamba, Biblia ilishuka kutoka Mbinguni na kuanguka moja kwa moja jinsi ilivyo (ambacho si kweli), anapaswa kukabiliana na mambo yanayohusu tamaduni.

2. Ebu sasa na tushughulikie mambo ya kimsingi. Namna tunavyoweza kutambua mambo ya kimsingi katika fungu la maandiko itatusaidia sana kutazama kiini cha ujumbe.

i. Ebu na tuiangalie Biblia kama kitabu chetu cha mafunzo katika mambo yale tungaliyaita ya kudumu kimsingi.

a. Hayabadiliki na inawahusu watu wote.
1) Kwa mfano "mwenye haki ataishi kwa imani."
2. "Mtumwa si mkuu kuliko bwana wake, wala aliyetumwa kuwa mkuu kuliko aliyemtuma."

ii. Tutawezaje kutambua kile ambacho ni cha kimsingi tukikifikia?
a. Kwanza kabisa jambo la kimsingi ni maelezo ya kawaida.
1) Kwa mfano:
a. Mwenye haki ataishi kwa imani
b. Mtumwa si mkuu kuliko bwana wake.
c. Hakuna nguvu isipokuwa Mungu.
d. Chachu dogo huchachua donge zima.
2) Ni ya kuhusu –ote kinyume na ile maalum.
a. Mwenye haki ataishi kwa imani inahusu -ote
1. Warumi 4:3 ni maalum kwa Ibrahimu
2. Ingawa Ibrahimu aliishi katika hali tofauti na watu wanaoishi leo hii, lakini alitajwa kama mfano wa kimsingi kwa watu wanaoishi leo hii anavyoelezea katika Rumi 1:17
i. Wewe na mimi hatuwajibiki kumtoa mwana watu wa kwanza kama sadaka ya kuteketezwa juu ya madhabahu ndipo tumfurahishe Mungu.
ii. Lakini kinacho tuhusu sote kanuni ya kimsingi.

iii. Mungu daima alihitaji imani yenye utii kutoka kwa wale wanaotaka kumpendeza.

3. Ukisha pata kanuni ya kimsingi, anza kukusanya vifungu vingi uwezavyo vyenye kufundisha mambo yanayofanana na pengine katika maneno tofauti.
i.) Warumi 3:28
ii) Waebrania 11:6 n.k.

4. Unapoendelea kujifunza maisha ya watu katika maandiko matakatifu, onyesha namna waliovyofaulu au kushindwa kufuata kanuni ya kimsingi.

b. Pili: ya kanuni ya kimsingi ni ya kujulisha ikionyesha kitu chenyewe.

1. Tafakari kanuni ya kimsingi iliyotolewa hapo juu.

c. Kanuni ya kimsingi zingine zinaweza kutumika kwa ushikamanisho mbali mbali.

1. Biblia inatufundisha k wamba, tunavuna tunacho kipanda.

i. Paulo anatumia kanuni ya kimsingi katika mambo ya kifedha.

a. 2Korintho 9:6

ii. Hosea 8:7

iii. Mithali 22:8

iii. Yesu alitumia neno mavuno akizungumzia roho za wanadamu

iv. zenye kusubiri kufundishwa na kuitikia injili.

d. Kanuni za kimsingi hazifungwi na agano lolote.

1. Warumi 1:17

2. Kuvuna na Kupanda

a. Hosea 8:7

b. Wagalatia 6:9

e. Kanuni za kimsingi hazibadili tu, bali hata hazibadilishwi.

1. Kuna vitu visyobadilika katika hali ya mambo yake.

a. Uzito (uzito), kutembea v itu kama nyota,mwezi, na jua, kutegemea vitu visiyoondoka, tegemeo la sayansi

i. Mtu anayejirusha kutoka orofa ya tano akitegemea kuanguka juu, atatambua jinsi sheria hii is ivyo badilika.

ii. Kanuni ya kimsingi ya kudumu, tuliokuwa tukiizungumzia, inaonekana kuwa haibadiliki.

b. Kuhusiana na mifano iliyotolewa na Troy Cummings, ebu na tuangalie ikiwa tutaweza kuamua ni kanuni ya kimsingi ipi tunayoweza kujifunza.

i. Kanuni ya kimsingi inayofundishwa katika Warumi 16:16 kuhusiana na “busu takatifu” ni kwamba, kusalimiana kwetu kati ya mtu na mtu kuwa kutakatifu.

a. Katika karne ya kwanza tabia ya kusalimiana ilikuwa ya kubusiana kwenye shavu la uso.

ii. Katika Yohana 13 katika Bwana kuwatawadha wanafunzi miguu, kanuni ya kimsingi imeelezewa katika Yohana 13:16:

1. Wanafunzi wa Yesu alitakiwa kujifunza kutokana na vitendo vya Yesu kwamba, walitakiwa kujishughulisha na vitendo vya kuhudumiana kwa unyenyekevu. Ikiwa Bwana aliwahudumia katika kitendo cha unyenyekevu hiki, wao wakiwa si wakuu kuliko yeye, wanapaswa kufanya hivyo.

2. Yohana 13:17

c. Hata ingawa 1Korintho 11:2-16 imetangazwa na wengi kuwa ni moja wapo ya vifungu vya maandiko vigumu kuelewa katika Agano Jipya, bado kuna kanuni ya kimsingi muhimu inayotakiwa kutambuliwa na kueleweka kirahisi.
   1. 1Korintho 11:3
   2. Chotechote Paulo alichokusudia kuelezea katika mazungumzo hayo yalikuwa na kusudi la kuonyesha mfano wa ukweli wa kanuni ya kimsingi iliyoelezewa katika 11:3

d. Moja wapo ya njia yenye uhakika ya kuthibitisha tendo au fundisho kuwa lina wafunga watu wa leo kinyume na kuwa tamaduni za watu ni kuangalia na kuona ikiwa inafungwa katika kile kinachojulikana kama “Utaratibu wa muumbo” (creation ordinances)
   i. Lakini Paulo anafunga mafundisho yake si katika tamaduni za watu za wakati ule bali katika mafundisho yaliyo yazamani.
   ii. Katika 1Timotheo 2:8-15 anatuelezea kwamba mafundisho yake kuhusu muundo wa mamlaka kati ya wanaume na wanawake ina mizizi yake katika:
      a. Utaratibu wa muumbo (mme na mke)
      b. Utaratibu wa kuanguka (Hawa ndiye aliyedanganywa.)

   iii. Mfano mwingine kuhusu pointi hii unapatikana katika mdahalo kati ya mafarisayo na Yesu kuhusiana na ndoa na kuoa tena.
      a. Walitaka kujua kama mwanaume alaikuwa na haki ya kumtalaki mke wake wa sababu yoyote.
      b. Yesu alitoa mafundisho ya Mungu yaliyo ya zamani katika kitabu cha Mwanzo 2
   iv. Yaliyo kuwa ya lazima na Yaliyojitokeza tu
      a. Kilicho karibu na ya (–ote na maalum) ni kuwa na ufahamu kuhusu tofauti kati ya lazima na ya kutokea tu.
      b. Katika Mdo. 10:48 tunasoma: “Akaamuru wabatizwe kwa jina lake Yesu Kristo....”
      c.. Hapa tunayo amri ya moja kwa moja kutoka kwa Mungu kwa mamlaka ya Kristo kupitia Petro. <u>Swali</u>: Je kulikuwako na yalitokea au yasiyo ya lazima kuhusiana na amri hii? Ilikuwako katika amri hii.
         1. Katika msitari 47,48 tunaona kwamba ubatizo

wa maji uliamuriwa. Hii ilikuwa ni ya lazima.

2. Lakini Petro hakuelezea kiasi cha joto cha maji au mahali pakupatikana maji hayo.(ya moto, ya baridi, yanayokwenda, yaliyo simama,mtoni, kisima, nje ya jengo, ndani ya jengo.)
3. Petro hakuelezea vitu hivi, na kujaribu kufunga vitu hivi vya kujitokeza au vya hiari, kuwa kielelezo cha lazima kufuata, ni dhambi.

d. Hii ni thibitisho kwamba, ya kutokea tu yanahusika katika utekelezaji wa yaliyo ya lazima.

2. Mungu ana amuru (fundisha) Wakristo kuimba nyimbo za rohoni na kushangilia moyoni (Efeso 5:19; Wakolosai 3:16)
   a. Ya lazima katika agizo ni kuimba jinsi Mungu alivyoelezea.
   b. Je, kuna yaliyojitokeza, yasiyo ya lazima yanayohusika na utekelezaji wa amri hii? Ndiyo. Mungu anatuamru kuimba(ya lazima), lakini ni wapi ametuelezea kwamba tuimbe :
      1. kwa kumia vitabu vya nyimbo mikononi;
      2. Bila vitabu vya nyimbo mikononi;
      3. Katika sehemu nne.
      4. Sauti 1, sauti 2, sauti, 3 na sauti 4
      5. Mmoja akiwa amesima mbele ya mkusanyiko au kama ameketi.
      6. Nyimbo walizotunga wazee na wahubiri wetu tu,
      7. Kwa utaratibu gani.
   d. Amri ya kuimba haina mojawapo ya hivi vitu maalum vya kujitokeza wala haiachi vingine.

   e. Kujaribu kuwafunga watu na vitu hivi ni kuongeza juu ya neno la Mungu, kufanya sheria mahali ambapo Mungu haja weka.

3. Amri ya kuhusu –ote na ya maalum:
   a. Sehemu hii imetolewa kutoka mafundisho ya Bw. Troy M. Cummings kule Southern Califonia School of Evangelism.
      1. Tunapaswa kutofautisha kutoka amri ya Mungu ya kuhusu –ote na ya kuhusu maalum.
      2. Kujaribu kufanya amri ya kuhusu -ote na kuifanya kuwa ya kuhusu maalum ni kupotosha neno la Mungu.

      3. Kujaribu kufanya amri ya kuhusu maalum kuwa ya kuhusu –ote pia ni kupotosha neno la Mungu.

4. Amri nyingi zinayo yote ya kuhusu –ote na pia ya kuhusu maalum. Tunapaswa kuacha iliyo ya kuhusu –ote k ubaki ya –ote na kuhusu maalum kubaki hivyo.

5. Tunaweza kwa urahisi kutambua ya kuhusu –ote na ya kuhusu maalum, tukijifunza kwa karibu alicho kisema Mungu kwa wangalifu; tusiongeze wala tusipunguze kile kilicho elezewa.

6. Mfano: Agizo Kuu (Mathayo 28:18-20; Marko 16:15-16; Luka 24:44-49)
   a. Vitu vingine katika agizo hili ni ya kuhusu –ote na vingine maalum.

   b. "Enendeni" ni ya kuhusu –ote hasa kuhusu namna ya kwenda, utaratibu wa kutumia katika usafiri.
   c. Kujaribu kubadilishi amri hii ya kuhusu –ote "enendeni" na kuifanya kuwa maalum kwamba kila anayekwenda anapaswa k wenda k wa usafiri wa merikebu, gari, au tembea kwa miguu, na kujaribu kufungu amri hizi juu ya watu, kama kitu cha lazima, badala ya kuwa uchaguzi wa anayekwenda, ni kulichezea neno la Mungu.
   d. "Fanya wanafunzi" au "fundisha" au "hubiri injili" inaelezea somo au kitu chenyewe cha kufundisha au kuhubiri; hii ni ya k uhusu maalum na haiwezekani kufanywa ya kuhusu -ote kwa kumaanisha namna yote ya injili.

   e. "Mkiwabatiza" linatokana na neno la Kiyunani <u>"Baptizo"</u> lenya maana ya "kuchovya" "kuzamisha" "kutumbukiza" haina maana ya "kunyunyiza" au "kumwagia" Katika Kiyunani kunyunyiza ni "Rantizo" mwaga ni <u>"Cheo</u>" mwagia <u>"ekcheo".</u>
   f. "Batiza" inazungumzia hasa "kutosa" neno kutosa haliwezi kumaanisha katika Kiyunani wala Kiswahili kunyunyiza au kumwagia. Amri ya Mungu maalum kukubali "kutoswa" haipaswi kubadilishwa, na kuwa ya kuhusu –ote na kukubali kufuata moja wapo ya kutoswa, kunyunyiza, na kumwagia.
   g. "Baptizo" katika Kiyunani maana yake ni "Kutosa" lakini haielezei ni kutoswa katika kitu gani, lakini maandiko mengine matakatifu (Mdo. 8:35-39; 10: 47-48) yanathibitisha mifano ya kibiblia kwamba watu walitoswa ndani ya maji. Kwa hiyo Mungu anatoa amri ya kutosa, na mifano ya Kimitume inaonyesha kwamba, ni kutoswa katika maji. Kwa hiyo Mungu anatumia amri ya moja kwa moja na mfano ya kimitume katika kutufundisha.
   h. Wakati "batiza" ni maalum ikiwa na maana ya kutosa na mfano wa Kimitume kutosa katika maji, lakini hakuna mahali katika maandiko matakatifu panapo elezea kiasi cha joto au usafi wa maji au maji hayo yapatikane wapi. Kwa hiyo mtu asilazimishe kufanya mambo kama hayo kama amri kutoka kwa Mungu.
7. Mfano wa amri ya Mungu inayohusu maalum ni kuimba; ku "imba" au "imba sifa" au "shangilia kwa Bwana moyoni mwako" (Efeso 5: 18,19; Wakolosai 3:16; Yakobo 5:13).

8. Kuimba ni <u>aina moja</u> ya muziki ni muziki wa <u>sauti ya moyo.</u>

9. Aina nyingine ya muziki inayoenda sambamba na muziki ya sauti ya moyo ni ile muziki inayotokana na chombo cha muziki, muziki unaotokana na chombo alichotengeneza mwanadamu badala ya sauti ya kibinadamu.

10. Katika Agano Jipya kwa matumizi ya ibada ya kanisa, Mungu hakutoa amri ya kuhusu -ote ku "fanya muziki" badala yake alitoa amri maalum ya aina moja ya muziki "kuimba kwa sauti ya kibinadamu, inayoambatana na sifa za kiroho za moyoni. Hii inaeleweka kwa urahisi. Mungu anataka sifa za kiroho za moyoni katika ibada, si za nje na sauti inayotokana na kitu au mlio wa nyuzi (kamba) Ni rahisi kwetu kama Yesu alivyoonya, kujaribu kumweshimu Mungu kwa vinywa "vyetu" wakati huo huo "mioyo" yetu ikiwa mbali naye. (Mathayo 15:8,9)

11. Kujaribu kubadilisha amri ya Mungu maalumu "kuimba" na kuwa ya –ote "kufanya muziki" ni kuwa na hatia ya kulipotosha neno la Mungu.

12. Hatupaswi kuongeza aina nyingine ya muziki kwa ule maalumu uliyoelezewa (wa sauti ya moyoni) kwa visingizio kwamba, Mungu hajatukataza kutumia "vyombo vya muziki" katika muziki wetu. Hii ni kuchukulia kwamba, ukimia wa Mungu ni ruhusa na kubadilisha neno lake na kuongeza juu yake. Kuongeza juu ya neno la Mungu ni makosa jinsi ilivyo makosa kuondoa juu ya neno lake.

13. Mungu hakusema, "hakusema kwamba, msitumie kahawa na bamunda (cake) katika "meza ya Bwana." Je, tunayo uhuru wa kuvitumia vitu hivi katika meza ya Bwana, Tofauti na vile maalumu Mungu alivyo agiza kutumia- mzao wa mzabibu na mkate? Hapana.

14. Je, Mungu alihitajika kutupangia orodha mrefu wa vyakula na vinywaji ambavyo hatukutakiwa kutumia tunapokula chakula cha Bwana? Hapana. Kwa nini? Kwa sababu alitoa aina maalumu ya kinywaji (maji ya mzabibu) na aina maalumu ya chakula mkate, alioupenda; kwa hiyo kwa kufanya hivyo, bila shaka alikuwa akikataa aina nyingine yote ya chakula na kinywaji.

15. Mungu alipotoa aina fulani ya muziki alioutaka, sauti, au kuimba, bila shaka hakuruhusu aina nyingine yote ya muziki ya vyombo vya kuundwa; haikuwa lazima kwake kutoa orodha ya vyombo, na kusema, usitumie ngoma, gitta, kinanda, n.k.

16. Katika Mwanzo 6:14 Mungu alimwagiza Nuhu kujenga aina fulani ya Safina yenye aina fulani ya mti- Mvinje. Kwa hiyo Mungu alielezea aina maalumu ya mti wa kutumia. Kama Nuhu angelijaribu aina ya mti alioielezea, na kutumia chuma, je! Jambo hili lingekubaliwa? Hapana.

17. Mti ulikuwa ni kifaa maalumu cha kutumia kinyume kabisa na chuma au aina nyingine ya kifaa. Kwa upande mwingine, mti nao unahusu –ote kwa sababu kuna aina nyingi ya miti. Lakini Mungu alikataa aina nyingine ya miti kwa kutaja "mvinje" Je! Mungu alihitajika kusema, usitumie, msonobari, mkalatusi, Mshita n.k.? Hapana. Aina maalumu ya mti aliouamuru, bila shaka ulikataza aina nyingine ya mti. Hili tunalifahamu.

18. Mungu akiamuru aina fulani ya tendo, (kama kuimba, muziki wa sauti), au aina fulani vifaa (kama mti wa mvinje) na mtu yeyote adhubutu kuongeza au aina nyingine ya kitendo, au vifaa, ni kupotosho moja kwa moja amri ya Mungu maalum aliyoitoa na kwa hiyo ni makosa. Ni

sawa na mtu anayejaribu kuondo agizo lolote maalumu alilolitoa Mungu. Pia ni sawa mtu anayetaka kubadilisha kitendo au kifaa.

19. Tuchukulie kwamba Nuhu alisema, “Nitatumia mti wa mvinje lakini ni taongeza mti wa msonobari kidogo kwa sababu msonobari ni mgumu kuliko mvinje na kwa hiyo utanisaidia katika ujenzi wa safina.” Sote tunapaswa kufahamu kwamba Mungu asingekubali msaada au nyongeza kama hiyo. Hicho kinachoitwa msaada kingelikuwa kuongeza mti mwingine tofauti na ule maalum Mungu aliokuwa ameagiza.
20. Kama tulivyozungumzia mahali pengine katika masomo yetu haya kwamba kuna misaada halali, au ya kujitokeza au ya hiari yanayofungwa pamoja katika utekelezaji wa amri ya Mungu na moja wapo wa misaada hii halali inaweza kutumika katika utekelezaji wa amri ya Mungu ya maalumu kuhusu tendo au kifaa kilicho amriwa.
21. Mifano: Mungu alipotoa amri ya mti wa mvinje, hakuna mahali alipoelezea kuhusu saizi ya mti ambayo Nuhu alitakiwa kutumia katika ujenzi wa safina. Nuhu alikuwa na uhuru wa kutumia saizi yoyote ya mti wa mvinje katika ujenzi wake wa safina. Alichotakiwa kutumia ni mti wa mvinje. Saizi ya mti ilikuwa ni hiari yake. Saizi ya mti isingeliweza kuongeza juu ya amri ya Mungu. Kwa sababu katika amri yake Mungu hakuelezea saizi iliyotakiwa. Kwa hiyo hakuna mwanadamu aliyekuwa na amri ya kutoa sheria kuhusu saizi ya mti Nuhu aliotakiwa kukata.
22. Katika kutekeleza amri ya Mungu kuhusu “imba” (aina ya muziki ya sauti ya maneno) hatuna uhuru wa kuongeza aina nyingine ya muziki.- kwa mfano vyombo vya muziki kwa madai kwamba vyombo vinatusaidia kutekeleza amri ya kuimba. Huo si msaada, kwa sababu unaingilia kitendo cha kuimba- unaacha amri na kuongeza kitu kingine juu yake.
23. Sasa kuna misaada ya hiari iliyo halali kuhusiana na kuimba ambao hauongezi juu ya tendo Mungu aliloamuru. Tunaweza kuimba tukiwa na kitabu, cha nyimbo mbele yetu, au bila kuwa na kitabu mbele yetu, hiyo ni hiari ya mtu. Tunaweza kufanya kinachotusaidia kama hiki. Kwa nini? Kwa sababu kutumia kitabu na kutotumia kitabu hakubadilishi amri ya Mungu ya “ku imba.” Kitabu ni moja wapo wa vitu vya hiari ni msaada unaokubalika. Kwa sababu Mungu hajasema ni msaada wa aina gani tuutumie. Kitabu cha nyimbo hakibadilishi aina ya muziki- unabakia muziki wa maneno.
24. Hatuwezi kutumia msaada unaotumia unaobadilisha amri yenyewe, misaada yote inapaswa kuwa kitu kinachotegemea amri yenyewe, kisichoingilia amri yenyewe.
25. Je mtu yeyote anayependa Kahawa na Bamunda (Cake) anao uhuru wakuchukuwa chakula na kinywaji chochote anachokipenda na kuongeza kwenye amri ya Mungu maalumu kuhusu chakula cha Bwana? Je, unaweza kuwa na haki ya kudai kwamba, hivi ni vitu vinanisaidia kula chakula cha Bwana? Hapana

F. MAPATANO YA KALE NA MAPYA(AGANO LA KALE NA MPYA)

1. Basi sheria ni nini? (Wagalatia 3:19)
2. Imeelezewa katika njia nyingi:-
   a. Kwanza tutambue kwamba torati ilikuwa nzuri.
      i. Warumi 7:16
      ii. Warumi 7:12- njema
      iii. Warumi 7:14- takatifu, haki, njema
   b. Katika hali ya lugha ya mfano imeitwa “kiongozi” “mwalimu”

Lakini wazo nyuma ya neno hilo lililotumika katika Wagalatia 3:23 ni sawa na mfano wa mtumwa aliyepewa wajibu na bwana wake kumpeleka mtoto shuleni.

i. "Mtumwa aliyekwenda na mtoto kutoka nyumbani kwenda shuleni katika lugha ya Kiyunani aliitwa "PAIDAGOGOS"
ii. Hii ndiyo iliyokuwa kazi ya sheria (torati)
iii. Kazi nyingine ya Paidagogos alitunza mtoto nyumbani na kumwongoza kwenda shuleni. (Galatia 3:24)

c. Sheria ya Musa pia inajulikana kama iliyokwenda kinyume na mwanadamu.
i. Wagalatia 5:1
ii. Mathayo 11:27-30
iii. Yesu alikuwa akizungumza na wale waliokuwa chini ya kongwa la sheria(torati)
iv. Wagalatia 3:13
v. Wakolosai 2:14

3. Itakuwaje sasa, sheria itaitwa njema, yenye haki, takatifu, na ya kiroho, iliyofanya kazi ya kuongoza, na tena ikaitwa laana na hati ya kutushitaki?

a. Sheria ilikuwa nzuri, yenye haki, takatifu na ya kiroho; kwa hiyo haikuwa na matatizo.
b. Warumi 8:3
c. Mwadamu hakushika sheria kwa sababu ya udhaifu wake.
d. Sheria yenyewe haikuwa dhaifu. Ilikuwa dhaifu kwa sababu ya ujinga wa mwanadamu.

4. Ni uhusiano gani Mkristo anaobakia nao kuhusu sheria(torati)?
a. Tunapaswa kuamua sheria walipewa nani?
i. Kutoka 19:1-5
ii. Kumbukumbu 5:3
iii. Wagalatia 3:11-25
iv. Kwa hiyo sheria walipewa Waisraeli tu, sio baba zao. Iliuwa ya kudumu hadi aje mzao.
b. Basi ni nini kilicho tendeka juu ya sheria ya Musa?
i. Waebrania 8:13
ii. Waebrania 7:12
iii. Waebrania 7:18
iv. Waebrania 10:9
v. Wakolosai 7:1-5
c. Ikiwa ineondolewa njiani, mwanadamu wa leo hashurutishwi kuitunza katika ukamilifu wake, isipokuwa katika kanuni ya kimsingi yake ndiyo inayotufunga.
i. Warumi 15:4
ii Ingawa sheria ilitundikwa msalabani, Paulo akiongozwa na Roho Mtakatifu anasema kwamba, tunajifunza katika mambo yaliyoandikwa.
iii. 1Korintho 10:6,11
iv. " " 10:6
v. Kutokana na historia ya Israeli, tunajifunza kwamba, hatutakiwi kutamani vitu ambavyo hatuhusiani navyo. (1Kor. 10:11)
d. 2Tim. 2:15-17
i. Ingawa mistari hii, inazungumzia kimsingi kanuni kuhusu maandiko yote matakatifu, lakini yalihusu Agano la Kale.

i. Yaliweza kuhekimisha mtu hadi kupata wokovu:

a. Yalionyesha dhamba kama “uovu” (Warumi 7:13)
b. Yaliwapa Wayahudi “ufahamu kuhusu dhambi.”
c. Yalifanya kama ramani ya kumwelekeza mtu kwa Kristo (Wagalatia 3:25) Yaliwaongoza Wayahudi kwa Yesu.

5. Fikiria ni mara ngapi waandishi wa Agano Jipya walinukuu matukio ya Agano la Kale bila kuwaelezea kwamba wanafungwa na sheria hiyo.
   a. Waebrania 11:1- 12:1
   b. Wakristo wenye asili ya Kiebrania waliandikiwa waraka huu, kwa sababu walikuwa wanaanza kurudia sheria kwa sababu ya mateso waliokuwa wakiyapata kutoka kwa Wayahudi.
   c. Kwa kuwatia moyo, mwandishi anaelezea watu wa Agano waliokuwa na imani. Kila mfano ulikuwa ni wakuwafanya wandugu hao kushikilia imani.
   d. Watu wa Agano la Kale kama Nuhu, Ibrahimu, Sara, Musa, na Rahabu walitajwa. (Waebrania 11:32)
6. Na ingawa hatufungwi na sheria za kipindi cha hawa watu walimo ishi, bado tunaangalia kama mifano ya kujifunza kimsingi.

   a. 2Petro 2:4-11 –Maonyo kwa watakatifu wa karne ya kwanza kuhusu manabii wa uongo waliojiingiza kwa siri kuleta uharibifu, Petro anageukia Agano la Kale kwa ajili ya mifano.

22/01/2002

1. Mungu hakuwaachilia watu waovu kipindi cha Nuhu bila kuwaadhibu kadhalika hata achilia waovu katika kizazi chochote.
2. Anawakumbusha kuhusu miji ya Sodoma na Gomora iliyogeuzwa kuwa majivu.
   a. Alifanya hivyo “akiifanya kuwa ishara kwa watu watakaokuwa hawamchi Mungu baada ya haya." (2Pt.2:6)
   b. Mambo ya kimsingi yanayofundishwa katika jambo hili, “Basi Bwana Ajua kuwaokoa watauwa na majaribu, na kuwaweka wasio haki katika hali ya adhabu hata siku ya hukumu.” (2Pt.2:9)
3. Katika kuwafundisha wanafunzi wake kuhusu maangamizi ya ghafula ambayo yangelitokea juu Hekalu, Yesu a lisema, “Kumbuka mke wa Lutu.”

b. Mifano:

1, Kuhusu habari ya kutotii Mungu kwa Adamu na Mkewe, tunajifunza nini?
   a. Kwa kufuata mazingira, amri ya kutokula mti wa matunda ya ujuzi wa mema na mabaya hatukupewa sisi.
   b. Lakini Adamu na Eva walionywa wasile, wangelikufa kama wangelikula, kwa hiyo walipokula, walikufa.
   c. Katika uasi wa amri hiyo,walikula na Mungu akawaondoa katika bustani ya Edeni mbali na mti wa uzima.
   d. Somo: Tunapaswa kutii maagizo ya Mungu.

2.Ebu na tuchukulie somo tunaloweza kujifunza kutokana na Ibrahimu na kuzaliwa kwa Isaka.
   a. Somo: (tusome katika Warumi 4:19-21) usikamanisho hutolewa kwa ajili yetu sisi..)
3. Nadabu na Abihu – Katika Walawi 10:1,2
   a. Walimtolea Mungu moto wakigeni (moto ambao Mungu hakuwa amewaagiza kutumia katika kuvukizia uvumba)

b. Fundisho la kimsingi: Watu wa leo wanapaswa kufanya tu kilicho amriwa na Mungu.

e. **U**sikamanisho katika vitendo na mambo ya kimsingi haya:

1. Mungu alimwamru Nuhu kujenga Safina, lakini, hajawahi kuamru mtu yeyote katika historia ya dunia amri kama hiyo.

2. Mungu alitoa sheria ya Musa au Agano la Kale kwa wajuku wa Ibrahimu takribani karne kumi na nne kabla ya kuzaliwa kwa Yesu, lakini sheria hiyo au Agano hilo halimfungi mtu wa leo yeyote awe Myahudi au Mtaifa (Tazama Galatia 3, Rumi, 7:1-7; Kol. 2:14-17) Soma pia kitabu kizima cha Waebrania.

4. Kunuku katika sheria za Agano la kale alizopewa Musa na kujaribu kufunga Wakristo nazo, ni upotovu mkubwa dhidi ya mapenzi ya Mungu.

5. Wengine husema, “Mungu habadiliki na kwa hiyo hawezi kubadilisha mapenzi yake, Yesu ni yule jan, leo, na hata milele.”

6. Hii ni kutokuelewa maandiko matakatifu sana. Tabia na uwezo wa Mungu havibadiliki, lakini Mungu amebadilisha baadhi ya sheria zake wakati mwingine. (Waebrania 7:12) tunasoma, “Maana ukuhani ule ukibadilika, hapana budi sheria nayo ibadilike.” Tazama pia Waebrania 8:6-12.

7. Agano Jipya la Yesu Kristo halikuweza kufanya kazi hadi kifo chake, (Waebrania 9:15-17). Mifano ya Yesu Kristo kipindi cha huduma yake binafsi jinsi alivyo waokoa watu si mifano yetu ya kufuata leo, kwa sababu wosia wake wa mwisho na Agano Jipya vilikuwa bado kuanza kufanya kazi.

8. Agizo la Kristo la mwisho na lililokuu kwa mitume na wanafunzi wake linalopatikana katika Mathayo 28:18-20;Marko 16:15-20;Luka 24:46-49) ambalo bila shaka ndiyo injili ya Kristo kwa Mataifa yote, haikuanza kufanya kazi hadi Pentekoste ya kwanza baada ya kufufuka na kupaa kwa Kristo akirudi Mbinguni kwa Baba. – Imeandikwa katika Matendo ya Mitume Sura ya 1& 2.

9. Kanisa la Bwana la kweli, katika kuanzishwa kwalo na kuenea inaelezewa katika kitabu cha Matendo ya Mitume. Hili ndilo Kanisa la asili, la zamani kuliko yote.- Lile alilolijenga kwa kupitia mitume wake walioongozwa na Roho Mtakatifu. Halikuwa, na bado si Katoliki, wala Protestanti., si madhehebu. Ndilo mwili mmoja, imani moja inayopatikana katika Efeso 4:1-6

10. Mtu hawezi kufahamu na kushikamanisha maandiko matakatifu impasavyo katika maisha yake na ya watu wengine kama hawezi kutofautisha maagano, sheria katika maandiko matakatifu.

F. Hatimisho na Muhutasari:

1. Hakuna maandiko ya Agano la Kale yanayoweza kuwafunga watu wanaoishi siku hizi katika hali maalum.—Isipokuwa maelezo kama hayo yanaweza kufunga watu leo kimsingi.

2. Kuna mambo ya kimsingi tunayoweza kujifunza kutokana na vitendo hivi.

a. Ili kumpendeza Mungu, wanadamu wanapaswa kutenda “kwa imani”

b. Kutenda kwa imani maana yake ni kwamba, mtu anatenda kwa kufuata neno la alilolisema Mungu.

i. Kwa kusikiliza maonyo

ii. Tusiondoe wala kuongeza juu ya neno la Mungu.

iii. Tusipotoshe neno la Mungu.

3. Imani pasipo matendo imekufa. (Kusikiliza maneno ya Mungu bila kufanya anavyosema ni dhambi na mshahara wa dhambi ni mauti.

4. Kufanya katika dini kile ambacho Mungu hajaamuru ni kuwa na hatia ya dhambi.

5. Mtu anaweza akafanya katika uaminifu wote (yaani akijisikia kwamba anachokifanya anamtii Mungu) kumbe yumo katika makosa.

G. Tofauti na kutopatana:

1. Ya kimsingi na ya –ote:

a. Biblia ni matokeo ya Roho Mtakatifu (2Petro 1:20)
b. Haiwezekani kwa Mungu kusema uongo.
    1. Tito 1:2
    2. Hesabu 23:19
    3. 1Samweli 15:29
    4. Waebrania 6:18
c. Moja wapo ya sheria za fikira huitwa “sheria ya kutopatana.”
    1. Katika asili, “Hakuna kitu kinachoweza kuwa kinaweza kuwa na kwa wakati huo huo kisiwe.”
    2. Aristotle alisema: “Haiwezikani kwa kitu kile kile kuwa kwa wakati moja kwa mtu mmoja kuwa katika njia tofauti.
    3. Mfano kutoka kwa mafundisho ya Bw. Thomas B. Waren: Hakuna kitu kianchoweza kuwa cheusi chote, na kisiwe cheusi kila wakati.
    4. Je, inawezekana Mungu kuwa na maana moja:
        a. Mwanzo 1:31
            1. Aliposema ni chema sana alikuwa akisema kwa wakati huo huo kuwa si chema?
            2. Mwanzo 6:6
        b. Wengine wanaweza kusema kwamba aliridhika na kwa wakati huo huo hakuridhika na kazi aliyokuwa ameifanya.
    5. Je, lugha inayotumika inafanana?
        a. Wakati wa kuongoka kwa Sauli watu waliosafiri naye inasemekana kuwa alisikia sauti iliyozungumza naye (Mdo.9:7)
        b. Lakini katika Mdo. 22:9 inasema kwamba, hawakusikia sauti.
        c. Hapa madai ha kupingana yanakuwa wazi.
            i. Katika Mdo. 9:7 Luka alichokuwa akisema ni kwamba sauti ilisikika..
            ii. Na katika Mdo. 22:9 anachosema ni kwamba hawakuelewa maana ya ile sauti walioisikia
        d. Katika hatimisho la marehemu Warren ni kwamba, maneno yanayoonekana kuwa hayaeleweki ni vema kutafuta uelewano badala ya kutoa madai ya kuwa Bibia inapigana.
    3. Katika kujifunza Biblia mwanafunzi anapaswa kuelewa mambo yafuatayo anapokabiliana na maneno magumu:
        1. “Shawishika kikamilifu akililini mwako kwamba fafunusi kamilifu ipo, ingawa hatujaipata.....”
        2. Shawishika kikamilifu kwamba Biblia ni maneno aliyoyasema Mungu Mwenyewe si habari za watu walizo andika kuhusu Mungu zenye udhaifu.
        3. Jifunze kwa wangalifu mazingira na muundo wa mistari yenye kuleta utata hadi upate ufahamu kuhusu kusudi la msitari. Ikikulazimu unaweza kujifunza kitabu kizima chenye msitari wenye utata, ukilinganisha maneno kama hayo kuwa yametumikaje katika sehemu zingine za maandiko matakatifu.
        4. Kumbuka kwamba, hakuna utafsiri wa maandiko matakatifu unaokubalika bila kuotoa nje maana ya maandiko kwa wangalifu. Maana yake ni kwamba

unapaswa kuamua alicho kimaanisha mwandishi na meneno aliyo yatumia.

5. Tumia kwa wangalifu vitabu kama kamusi ya Biblia, Encyklopedia za Biblia.

D. Ya wazi na Isiyo ya wazi (ya kumaanisha):

1. Yote yanayofundishwa na Biblia yanafundishwa kwa njia ya wazi na kwa njia ya kumaanisha.
   a. Ya wazi ni yenye mistari iliyotolewa maelezo ya maandiko matakatifu kuanzia kitabu cha Mwanzo 1:1 hadi Ufunuo 22:21
   b. Ya kumaanisha ni yale yanayoeleweka kutokana mistari ile iliyotolewa.

E. Hatimisho:

1. Ni muhimu kwa mwanafunzi wa Biblia kufahamu tofauti kati ya:
   a. Ya kudumu na ya muda. (miujiza, lugha, unabii)
   b. Ya utamaduni na ya kimsingi (Kuwatawadha wanafunzi-Yon.13:12)
   c. Ya lazima(ya asili) na isiyoyalazima(iliyotokea tu) (Mdo. 20:7-12)
   d. Ya -ote na ya maalum (Marko 16:15-16)
   e. Agano la Kale na Agano Jipya.
   f. Tofauti na ya kupingana.
   g. Ya wazi na ya kumaanisha.

G. Mtu anatakiwa kufikia hatimisho tu baada ya ushahidi wa kutosha (Sheria ya kulingana na akili)

1. Hii ni wazi kwamba hata katika kanisa la Bwana kuna wanaopinga kwamba katika kuelewa biblia akili za kibinadamu zinatakiwa kuwa kama kielelezo cha Mungu.
   a. Akili za kibinadamu hazitakiwa kupinga alichokisema Mungu, wala kutumika badala ya neno la Mungu.
   b. Je, neno la Mungu, ambalo ndiyo mamlaka ya mwisho, linaweza kueleweka bila mtu kutumia akili Mungu alizo mpa? Haiwezekani.
   c. Kwa hiyo tunaposema kwamba akili za kibinadamu zinahitajika tuna maana kwamba ili mtu apate kuelewa neno la Mungu lazima atumie akili zenye maantika ili kufikia hatimisho.
   d. Akili za kibinadamu kwa njia ya mantiki ni ya lazima kwa kufahamu maandiko matakatifu.
   e. Akili za kibinadamu zikibatilisha hali ya kukubaliwa kwa mifano, au matukio yaliyotendeka, kujua jambo kwa kuijua sababu, kwa hiyo pia itabatilisha hali ya Mungu ya amri ya moja kwa moja ya vitu kama maonyo, maswali, maelezo ya wazi, na maelezo yenye masharti.
   f. Points zenye mifano:
      1. Katika mdahalo kati ya Bw. Connally, na Hicks, Olan Hicks alimuliza Connally kwamba, “Ikiwa katika utaratibu wako wa kutumia maantiki, unafikia hatimisho inayopingana na mafundisho ya wazi ya ukweli wa Biblia, utafuata nini? Utafuata maelezo ya Biblia au utafuata hatimisho ya maantiko yako?
      2. Kwa usahihi Connally alijibu kwa kusema: “Maantiki sahihi, yenye kutokana na habari sahihi, haiwezi kukufikisha kwenye hatimisho makosa.

H. Sawa na ukweli wote, uwezo na haki ya kujifunza na kufahamu maandiko matakatifu, ni kwa mtu binafsi.(sio “kanisa” viongozi kukufanyia utafsiri) hiyo inaweza kutumika vibaya.

1. Hii haina maana kwamba kila mtu anayo uwezo wa kufahamu maandiko matakatifu ulio sawa na wa mwingine.
2. Bila shaka watu wengine wanayo akili ya kuzaliwa, elimu bora, na uwezo wa kujifunza na kufahamu vitu vya ndani katika maandiko matakatifu kuliko wengine. Maandiko yanaonyesha kwamba watu binafsi wanao uwezo tofauti (Mathayo 25:14-30) kila mtu amepewa uwezo kadhaa.
3. Hakuna mtu aliye na haki ya kufikia hatimisho anayoitaka yeye mwenyewe.
4. Unyenyekevu wa kutosha utamfanya mtu alinganishe fikira zake na za wanafunzi wa Biblia wengine. Kuwa tayari kujifunza kwa wengine badala ya kulazimisha mawazo yako pekee.

J. Mtu anapaswa kutambua kwamba kuna vitu ambavyo ni vigumu kuvielewa.
1. Sote tunakubaliana kwamba vitu vyote katika Biblia ni wazi na rahisi kufahamu.
2. Kwa huo huo, Mungu alifanya vitu vingine kuwa vigumu kuelewa (2Pt.3:16) Alikuwa na kusudi lake kwa kufanya hivyo, labda alitaka tujibidishe katika kupata baraka zetu za kiroho.

**********Mwisho 12/02/2002

3. Kuna vifungu vingi katika maandiko matakatif ambavyo ni vigumu sana kwetu kuelewa maana kamili siku hizi.
4. Watu wengine hawafahamu kwamba k una vifungu vigumu kama hivi, wanaamini kwamba hawajajifunza vya kutosha.
5. Wengine wameruka haraka na kufikia hatimisho yao na kuona kwamba hakuna tatizo kwa sababu ya ufinyu wa kujifunza kwao.
6. Bila shaka wote wanaotafuta vyakutosha, watafahamu maandiko matakatifu na kupata wokovu. Ebu sote na tuwe na moyo wa kuendelea kukua kama Petro alivyo sema, “Lakini kueni katika neema na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo. Utukufu una Yeye sasa na hata milele.

K. Kujifunza kwa mazoea: Mafunzo ya Mathayo 24
1. Wanafunzi walikwenda kwa Yesu kwa faragha wakisema, “Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini? Nayo nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia?” (Mathayo 24:3)
   a. Katika sura iliyotangulia, Mathayo 23, Yesu alikuwa tayari ametanga Ole 8 akiwa laani waandishi na mafarisayo wa siku zake.
      i. Alikuwa amewashambulia kwa sababu ya maisha yao ya kujionyesha na ya u nafiki, kukosekana kwa nia sahihi na kukosa kukazia kilicho sahihi.
      ii. Katika kutangaza ole ya mwisho alisema, “Kijazeni basi kipimo cha baba zenu. Enyi nyoka ,wana wa majoka, mtakimbiaje hukumu, ya jehanam? Kwa sababu hiyo, angalieni mimi natuma kwenu manabii na wenye hekima, na waandishi, na wengine wao ninyi mtawaua na kuwasulibisha, na wengine wao mtawapiga katika masinagogi yenu, na kuwafukuza mji kwa mji; Hivyo ije juu yenu damu yote ya haki iliyomwagika juu ya nchi, tangu damu ya Habili, yule mwenye haki, hata damu ya Zakaria bin Baraka,mliyemwua kati ya patakatifu na madhabahu. **Amini, namwaambieni**, **Mambo hayo yote yatakuja juu ya kizazi hiki.”** (Mathayo 23:32-36)
      iii. Na kilio chake juu ya ukosefu wakupata uitikio kutoka Yerusalemu, alisema, “Angalieni nyumba yenu mmeachwa hali ya ukiwa.” (Mathayo 23:38)
   b. Katika Sura 24 Yesu anaonekana akiondoka hekaluni.
      (1) “.....wanafunzi wake wakamwendea ili kumwonyesha majengo ya hekalu.” (24:1)

(2) Lakini walipokuwa watamani uzuri wa majengo yenyewe, Yesu alisema, "....Halitasalia hapa jiwe juu ya jiwe ambalo halitabomoshwa. (24:2)

(3) Alipokuwa amekwenda kwenye Mlima wa Mzeituni wanafunzi walikwenda kwake faraghani wakitafuta maelezo zaidi kuhusu hekalu.

c. Katika mafunzo sambamba ya Mathayo 24 na Marko 13 na Luka 21, inaonekana wazi kwamba, maswali yaliyoulizwa yalikuwa mawili:

(1) Hekalu litaangamizwa lini?

a. Na ni nini ishara wakati wa kukaribia kuangamizwa kwa hekalu? (Luka 21:7, Marko 13:4)

(2) Utarudi lini?

a. Na ni nini ishara zitakazotangulia kurudi kwako?

d. Kimakosa wanafunzi wake walifikiria kwamba, kubomolewa kwa hekalu na kurudi kwake mara ya pili vitakuwa wakati mmoja.

(1) Lakini haifuati hivyo, kwa hiyo walivyodhani sivyo ilivyo kuwa.

(2) Kabla hatujaanza kukata kati somo letu, kuna ponti moja au mbili.

a. Kuna maswali mawili yaliyoulizwa, aina mbili ya kurudi ikazungumziwa, na mwisho mbili ikafunuliwa.

i. Kurudi kwake katika kuhukumu Yerusalemu iliashiria mwisho wa Dini ya Kiyahudi na Taifa la Kiyahudi.

ii. Kurudi kwake katika hukumu ya mwisho iliashiria mwisho wa dunia.

b. Pili, ningependa mfahamu kwamba, jibu kamili kwa wanafunzi linaendelea katika 24 na 25.

(3) Muhutasari wa mazungumzo yetu:

a. Kuhusiana kubomolewa kwa Hekalu na mwisho wa taifa la Kiyahudi:

i. Tutatazama ilikuwa itendeke lini.

ii. Tutatambua zilizo kuwa ishara ya kuja kwa kubomolewa kwa Hekalu.

b. Kuhusiana na mwisho wa dunia:

i. Tutazama ilikuwa itendeke lini.

ii. Tutatambua zitakazo kuwa ishara zake.

c. Kwa mtindo kama huu, tatachunguza jibu Yesu alilolitoa kuhusu maswali mawili alioulizwa na wanafunzi wake Mlimani Mzeituni (Mathayo 24:3)

(4) Kubomolewa kwa Yerusalemu:

a. Hekalu lenyewe lina Historia ndefu na inayotofautiana.

i. Kwanza ilijengwa na Sulemani (967-960 K.K.) na kubomolewa na wa Babeli katika mwaka wa 586 K.K.

ii. Wakati Wayahudi waliokuwa uhamisho walipokuwa wamerudi. Chini ya agizo la mfalme wa Ajemi Koresho Hekalu la pili lilijengwa.(Katika kipindi hiki tunao Ezra, Nehemia, Haggai, na Zakaria.)

iii. Ukarabati wa Hekalu la pili, ulianza katika 20 K.K. na Herode Mkuu na ulikuwa ukiendelea hata kipindi cha huduma binafsi

wa Yesu.(Wakati mwingine hili huitwa hekalu la tatu.)

a. Yohana 2:20 tunaelezewa kwamba lilichukuwa miaka 46 kujengwa.

b. Ukarabati huu haukumalizika hadi mwaka wa W.K. 64

c. Mwishowe, Hekalu hili liliharibiwa na Warumi katika mwaka W.K. 70.

b. Yesu aliposema kwamba, hekalu litabomolewa, na hakutasalia jiwe juu ya jiwe, wanafunzi walitaka kujua ni lini itatendeka.

(1) Mst. 4—35 inayo jibu la kwanza.

(a) Katika mstari wa 34 Alisema, "Amini na waambia, Kizazi hiki hakitapita, hata hayo yote yatakapotimia. "

(b) Hayo yote nini? Hayo yote aliyokuwa ametangulia kusema.

(c) Ebu na tuchunguze mistari hii:

1. Kwanza kabisa, Yesu alitoa mlolongo ya ishara zitakazo onekana kuhusu kuja kwa kuangamizwa kwa Yerusalemu.

a).Makristo wa uongo wangelikuja na kuwapotosha walio wengi. (mst. 5)

b)Kungelisikika habari ya vita na matetezi za vita.(mst.6)

c)Taifa litainuka juu ya taifa,ufalme juu ya ufalme(mst.7)

d)Kungelikuwa na majanga ya asili kama njaa, tetemeko la ardhi(mst7)

e)Mateso makuu yangelitokea juu ya kanisa (mst.9)

f)Manabii wa uongo wangeliinuka na kupoteza wengi (mst.11)

g)Injili ingelihubiriwa duniani kote kwa ushuhuda wa mataifa yote.(mst.4)

h)Chukizo lingetokea (mst.15)

3. Katika (mst.6) "nanyi mtasikia habari za vita na matetesi ya vita; angalieni msitiswe; maana hayana budi kutukia lakini ule mwisho bado."

a)Mwisho wa nini? Katika mazingira yetu, mwisho Yerusalemu.

4. Zingatia: mst. 8 "hayo yote ndiyo mwanzo wa utungu."

5. Na katika mst.14- "tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika Ulimwengu wote, kwa mataifa yote hapo ndipo ule mwisho utakapokuja." (mwisho wa Yerusalemu)

e. Inaonekana mst. 15 ndiyo mahali petu pa kugeukia ili tufahamu jambo hili: "Basi hapo mtakapoliona chukizo la uharibifu, lile lililonenwa na nabii Danieli, limesimama katika patakatifu (asomaye na afahamu),"

1. Walitakiwa kufanya nini watakapoona chukizo la uharibifu?

(a) "Ndipo wilio katika Uyahudi na wakimbilie milimani."

(b) "Naye aliye juu ya dari asishuke kuvichukua vitu v ilivyomo nyumbani mwake;"

(c)"wala aliye shambani asirudi nyuma kuichukua nguo yake."

(d) Walitakiwa kuomba kwamba, k ukimbia kwao kusiwe katika wakati wa baridi wala siku ya sabato.

(e) "kwa kuwa wakati huo kutakuwako dhiki kubwa, ambayo haijatokea namna yake tangu mwazo wa ulimwengu hata

sasa,”

ZINGATIA: Kama hii ingelihusu kurudi kwa Yesu mara ya pili, kukimbilia milimani kungeliwasaidia nini n.k?

3. Chukizo la uharibifu lilikuwa nini?
   (a) Ilikuwa ndiyo ishara kuu ya kuwaonya Wakristo wa wakati ule kuondoka Yerusalemu haraka kutokana na mateso yaliyokuwa yakija.
   (b) Mistari yetu ya usambamba itatutambulisha ishari kuu hizi:
   1. Luka aliandika, “Lakini hapo mtakapoona mji wa Yerusalemu umezungukwa na majeshi, ndipo jueni ya kwamba uharibifu wake umekaribia.” (21:20)
   2. Ishara zote za awali zilifananishwa utungu wa mwanamke,lakini chukizo la uharibifu lili ashiria mwanzo wa mwisho na mateso makuu juu ya Wayahudi ambayo ilikuwa haijawahi kutokea katika historia.

b. Chukizo la uharibifu maana yake ni mateso ya majeshi ya Warumi.
c. Josephus, mwana historia wa Kiyahudi, aliandika kwamba, mahali patakatifu penyewe paliharibiwa kwa moto pamoja na majengo yote yaliyo ya zunguka.
d. Walileta wakuu(miungu) wao katika Hekalu na kuwatolea dhabihu.

3.Fikiria uchangunuzi kutoka kwa Josephus:
   a.)Baada ya k uangamizwa kwa Yerusalemu:
      1)Wafalme wa Rumi 4 waliwaua kinyama
      2)Wayahudi 50,000 walichinjwa kule Seleukia.
      3)Wayahudi 20,000 walichinjwa Kaisaria
      4)Kumbuka vita na matetezi ya vita na njaa vilikuwa utungu tu.
   b)Maangamizi ya Yerusalemu ingelikuwaje?:
      1) Wayahudi 79,000 walichukuliwa mateka.
      2) 1,000,000 walikufa wakati wa kuhusuru.
      3) Wa mama waliwatokosa watoto wao ili kupona na njaa.
   c)Yesu aliwaonya pia kuhusu ishara za uongo:
      1)Wengine wangelisema, “Tazama Kristo yuko hapa,”
      2)Yesu alisema, “msiwaamini.”
         a)Katika msitari wa 27 anaelezea kuhusu kurudi kwake mara ya pili. “Kwa maana kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi, hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu.”
         b)Katika maneno mengine alikuwa akisema, hatakuja kwa kujificha, ataonekana ulimwenguni kote.

f. Tulijifunza kwamba, kuna kurudi kwa aina mbili katika 24, 25.

1. Kutaja tu kuja kwa Bwana hakuna maana ya kuthibitisha kwamba alikuwa akizungumzia kurudi siku ya mwisho.
    a. Katika mistari 29-31 tumeelezea kurudi kwa Bwana katika hukumu.(SOMA).
    b. Zingatia: Mst. 30 “Ndipo itakapoonekana ishara yake mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni ndipo mataifa yote ulimwengu wataomboleza, nao watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi.”
    c. * Maneno haya: ***<u>“Nao watamwona mwana wa Adamu akija juu ya mawingu mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi.”</u>***
2. Kwa kusikika hii inaonekana kuwa kurudi kwa Yesu mara ya pili, lakini zingatia lugha inayouzunguka msitari huu.
    a. Mst. 29 “lakini baada ya dhiki ya siku zile, jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake, na nyota zitaanguka mbinguni, na nguvu za mbinguni zitatikisika.”
    b. Mst. 34 “Amini na waambia kizazi hiki hakitapita, hata hayo yote yatakapotimia.”
3. Tuangalie pia mistari mingine yenye lugha kama hii,.
    1) Isaya 19:1 “Ufunuo juu ya Misri. Tazama, BWANA amepanda juu ya wingu jepesi, anafika Misri, na sanamu za Misri zinatikisika mbele zake, na moyo wa Misri unayeyuka ndani yake.
    2) Isaya 34:4,5 “Na jeshi lote la mbinguni litafumuliwa, na mbingu zitakunjwa, kama karatasi, na jeshi lao lote litanyauka kama vile jani la mzabibu linyaukavyo na kupukutika, na kama jani la mtini linyaukavyo na kupukutika. Maana upanga wangu umekunywa na kushiba mbinguni;tazama utashuka Edomu na kuwahukumu.”
    3) Lugha kama hiyo pia inapatikana katika Ezekieli 32:7,8 “Nami nitakapokuzimisha, nitazifunikiza mbingu, na kuzifanya nyota zake kuwa giza; nami nitalifunika jua kwa wingu wala mwezi hautatoa nuru yake. Mianga yote ya mbinguni ingazayo nitaifanya kuwa giza juu yako, nami nitatia giza katika nchi yako asema Bwana MUNGU.”
        a. Hapa alikuwa akizungumzia kuhusu hukumu juu ya Misri.
    4) Mistari hii yote haizungumzii kuhusu kurudi kwa Bwana mara ya pili.

    5) Katika Agano Jipya tunaweza kutazama katika zile barua walizoandikia makanisa saba ya Asia katika Ufunuo 2,3.
        a)Aliliambia kanisa la Efeso kutubu “.....naja kwako, nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu” 2:5.

g. “Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kamwe.” (mst. 35)
    1). Ninaamini kwamba mst. Wa 36 unatakiwa kufahamika kama msitari wa kutuhamisha. “walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake.” (24:36)

(2).Angalia kwa makini maandishi inayopatikana katika sura 23 na 24:1-35:

a. 23:36, “...mambo hayo yote yatakuja juu ya kizazi hiki.”
b. “Hamwoni haya yote,”
c. “Tuambie mambo hayo yatakuwa lini?
d. “Kizazi hiki hakitapita, hata hayo yote yatakapotimia.” (24:34)

(e)MSITARI WA KUHAMA: “Walakini habari ya siku ile na saa ile, hakuna ajuaye, hata malaika wa mbinguni, wala Mwana ila Baba peke yake.

1. Siku mbingu na nchi vitakapo pita.

5. Mafundisho ya Yesu kuhusiana kuja kwake mara ya mwisho:

a.) Kuhusiana na swali “Lini” alisema, hakuna ajuaye ila Baba.

b.) Kuhusiana na ishara kabla ya kuja kwake, hakutakuwa na ishara.

1) “kama ilivyo kuwa siku za Nuhu, ndivyo kutakapokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu.” (24:37)

2) Kabla ya gharika walikula na kunywa, walikuwa wakifurahi, wakioa na kuolewa hadi ilipofika siku ya Nuhu kuingia safinani, hawakujua hadi gharika ilipokuja na kuwaangamiza..

(a)Ndivyo itakapokuwa siku ya kuja kwa Mwana wa Adamu.

3) Kwa hiyo Yesu aliwashauri, “Kesheni basi, kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu.”

a) 1Wathesalonike 5:2

b) 2Petro 3:10

4) Tofauti kubwa inapaswa kutambulika kati ya kurudi kwake na kuangamizwa kwa Yerusalemu.

a) Kulikuwa na ishara walizopewa kuwaonya watakatifu kuhusu kuangamizwa kwa Yerusalemu.

b) Lakini hakuna ishara walizopewa kuhusu kuhusu kurudi kwake mara ya pili.

1. Siku kabla ya kurudi kwa utukufu wake mara ya pili, watu watakuwa wakiendelea na shughuli zao za kawaida.

5) Kwa sababu hakutakuwa na ishara, Yesu alitaka watu wote “kukesha” na “kuwa tayari”

a) Sura 25 inayo pointi kuu tatu:

1)Mfano wa wanawili kumi mistari 1-13 somo kuhusu “utayari.”

2)Mfano wa talata 14-30 somo kuhusu matumizi mazuri ya muda na talata zetu.

3)Kurudi kwa Yesu mara pili kumeonyeshwa kama kutenganisha kondoo na Mbuzi. (mistari 31-46)

a.Kwa wenye haki atasema, “Njooni ,mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu.” (25:34)

b.Bali kwa wasio haki, atasema, “Ondokeni kwangu mliolaaniwa mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake.” (25:46)

6) Muhutasari:

a). Kuhusu kurudi kwa Bwana kuhukumu Yerusalemu na mwisho wa taifa la Kiyahudi.

1. Hasa kuhusu wakati wenyewe, ungelikuwa wakati wa kizazi kile.
2. Hasa kuhusu ishara zingelikuwa:
   a. Zenye kupoteza
   b. Zenye kuwafanya wenye haki kutoroka.

b. Kuhusu kurudi kwa mara ya mwisho kwa Bwana kuhukumu kuonyesha mwisho wa ulimwengu:

1. Kuhusu wakati wa kurudi kwake,-- Ni Baba peke yake anayejua.
2. Kuhusu ishara- Hakutakuwa na ishara zozote.

I. LUGHA YA MFANO:

A. Nini maana ya lugha ya mfano?

1. Wakati neno limetumika kumaanisha jambo fulani na baadaye kuhamishwa litumike kwa kuakilisha jambo lingine, inasemekana kuwa limetumika katika ***lugha ya mfano***.
2. Neno linapotumika katika maana yake ya asili, hilo neno limetumika katika ***lugha halisi***.
3. Kwa hiyo, lugha ya mfano ni kuhama kutoka katika maana ya asili au ya zamani iliyo ya kawaida.
4. Katika lugha zote, lugha ya mfano hutumika kuelezea mawazo ya watu wenye busara.

5. Lugha halisi inaweza kupatikana katika karibu kila lugha kwa kuelezea mawazo kama, chuma *baridi*, sakavu *ya mawe*, mbao *ngumu*, udongo *mlaini.* Lakini hakuna lugha inayoweza kuelezea mawazo kama, moyo *baridi*, moyo *wa mawe*, moyo *mgumu*, moyo *mlaini.* Kuhusu moyo, vivumizi jina hivi huzungumza katika lugha ya mfano.

a.)Ni kwa sababu lugha halisi ilitumika kwa kuelezea kitu kisicho na uhai na maneno hayo hayo ya kitumika kuelezea kitu cheny uhai, huwa ni lugha ya mfano. (Mathayo 3:5) *nchi zote* ni lugha ya mfano. Nchi haitembei kwa hivyo alikuwa na maana watu wa nchi hizo walimwendea Yohana.

B. TUTAJUAJE KAMA LUGHA NI YA MFANO:

1)Katika lugha halisi neno likionekana kuwa si la kawaida, ama haliendani sawa na sehemu zingine katika sentensi, tunaweza kuhatimisha kwamba, lugha iliyotumika hapo ilikuwa lugha ya mfano. (SOMA Mathayo 3:5) "Ndipo **wa**lipomwendea Yerusalemu na Uyahudi **wote** na nchi zote kandokando ya Yordani." Viakilishi jina "wa" na "wote" huonyesha kwamba waliomwendea walikuwa watu, kwa hiyo neno **"nchi zote"** ni lugha ya mfano yenye maana watu wote wakazi wa nchi kandokando ya Yordani.

C. KANUNI # 1. Pendekezo la ya lugha halisi.

1)Kwa sababu lugha halisi ndiyo inayotumika sana katika matumizi ya kawaida, kila neno litachukuliwa kwanza kama la lugha halisi, hadi itakapoonekana sababu nzuri ya kulifanya lisiwe hivyo.

2)Mfano mzuri mwingine kuhusu jambo hili ni neno "batiza" katika (1Korintho 15:29) "Au je! Wenye kubatizwa kwa ajili ya wafu watafanyaje? Kama wafu hawafufuliwi kamwe, kwa nini kubatizwa kwa ajili yao." Neno "Batiza" mara nyingi hutumika katika lugha halisi sawa na jinsi Yohana alivyo wabatiza watu ama kipindi cha mitume walipopewa amri ya kwenda kubatiza ili kuwaingiza watu katika ufalme wa Kristo. Lakini kwa wakati mwingine neno hili limetumika katika lugha ya mfano sawa na jinsi Yohana alivyosema, kubatizwa katika Roho Mtakatifu na katika moto, au kama Yesu alivyowaambia wana wa Zebedayo kwamba watabatizwa katika ubatizo wake akiwa na maana ya mateso yake. (Mathayo 20:22,23; Marko 10:38,Luka 12:50)

HERMANUITIKSI
MTIHANI WA KWANZA
MWAKA 2001
MHULA 1
MKUFUNZI: Francis Wechesa
JINA LA MWANAFUNZI_____03/05/2001

1. Hermanuitiksi ni nini?_____

2. Namna ya kutumia Hermanuitiksi huitwa nini?_____

3 Kusudi la exegesis ni kufanya nini?_____

4. Hermanuitiksi halisi ni muhimu kwa sababu itatusaidia kuelewa vema mambo haya:

   1. _____

   2. _____

   3. _____

   4. _____

KATI YA MAMBO YA MSINGI KUMI YALIYO MUHIMU KUTUSAIDIA KUFAHAMU MAANDIKO MATAKATIFU TAJA MATANO:

1._____
_____
_____
_____
2._____
_____
_____

3._____
_____

HERMANUITIKSI
MTIHANI WA PILI
MWAKA 2001 MHULA 1
MKUFUNZI: Francis Wechesa
JINA LA MWANAFUNZI_____17/05/2001

1. Kuna mambo mangapi ya msingi yaliyo muhimu katika kutosaidia kufahamu maandiko matakatifu? A. Saba B. Kumi na moja C. Kumi.

2. I kiwa mwanadamu anaweza kufahamu kwamba Mungu yupo, kwamba, Biblia ni neno la Mungu, na kwamba, Biblia inafundisha kwamba, Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, na kwamba kuokolewa kutoka dhambini, mwanadamu anapaswa kuamini katika yeye,kumpenda, na kumtii, basi:

   A. Mwanadamu hawezi kufahamu kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, na kufahamu kwamba, ili kuokokolewa kutoka dhambini, mwanadamu anapaswa kumwamini, kumpenda, na kumtii.

   B. Mwanadamu anaweza kufahamu kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, na kufahamu kwamba, ili kuokolewa kutoka dhambini, mwanadamu hanapaswa kumwamini, kumpenda, na kumtii.

   D. Mwanadamu anaweza kufahamu kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, na kufahamu kwamba, ili kuokolewa kutoka dhambini, mwanadamu anapaswa kumwamini, kumpenda, na kumtii.

3. Kama Biblia si neno la Mungu basi haina kanuni ya moja kwa moja kuhusu nini?
   A. Maisha yetu. B. Dhambi. C. A na B ni sahihi.

4. Vitu vya kuzingatia kuwa Biblia imetoka kwa Mungu:
   A. Unabii na Utimilifu wake, umoja, kutoweza kuhabiwa kwayo, usahihi wa hitoria, usahihi wa Sayansi.
   B. Umoja, Kutoweza kuzeeka kwayo, usahihi wa historia, Hisabati na sayansi, unabii na utimilifu wake.
   C. Usahihi wa historia, Sayansi, unabii na utimilifu wake, kutokuelewana kwayo katika sehemu zingine.

5. Katika Tito 1:2 na Waebrania 6:18 imethibitisha kwamba, biblia hawezi kufanya nini?

   A. Kuwa neno la Shetani, B. Kusema ukweli kila sehemu,, C.Kusema uongo.

6. Maandishi ya asili ndiyo nini ya mwisho? A. Maandishi ya mwisho, B. Mamlaka ya mwisho. C. Ndiyo tafsri tu.

6. Agano Jipya la Kiyunani ndiyo Agano Jipya, vingine vyote ni nini?
   A. Maandishi tu, B. Ni tafsiri tu, C. Uongo mtupu.

7. Ili mtu awe na usikivu wa kiroho, anapaswa kuwa mnguana kiroho vyakutosha, ili kuweza kupokea neno la Mungu na nini?

   A. Na bidii na uvumilivu B. Na Uelekevu wa moyo C. Na maombi na Sala

8. Ili mtu kuwa na usikivu wa kiroho, anapaswa kujinyenyekeza kama nani anapojifunza na kusikia neno la Mungu? A. Kama mtu mnguana B. Kama mtoto mchanga C. Kama mhubiri.

9. Ili mtu kuwa na usikivu wa kiroho, anapaswa kuwa mtu anayetawaliwa na Roho wa:

   A. Uvumilivu. B. Ukweli, C. Wa kunena.

10. Ili mtu kuwa na usikivu wa kiroho, mtu anapaswa kutambua kwamba, laana ya Mungu ni juu ya wale wanaolifanya nini neno la Mungu?

    A. Wanao lizingatia B. Wanao lipotosha C. Wanaolizingatia.

11. Watu wengine hawawezi kugudua ukweli uliofichika unaopatika katika biblia kwa sababu:
    A. Hawana Roho Mtakatifu, B. Hawajifunzi kujifunza kwa undani C. Ni wenye dhambi

12. Sababu zingine zinazowafanya watu kukosa hazina iliyofichaka hii ni:

    A. Upofu wa kiroho, ulemavu wa kiroho, Uwiano makosa, Umadhehebu,
    B. Umadhehebu, Kukosa bidii, Uwiano makosa, upofu wa kiroho.
    C. Uwiano makosa, upofu wa kiroho, umadhehebu, utofu wa nidhamu.

13. Hazina hii imefichwa kwa kusudi gani?

    A. Kwa sababu Mungu anatafuta walio na njaa na kiu ya neno lake, ili watu wasio watakatifu na wenye busara wasilichezee na kuligeuza kitu cha kawaida.

    B. Kwa sababu Mungu anataka watu wapokee Roho mtakatifu, ambaye ndiye atakayewafunilia hazina hii iliyofichika.

C. Kwa sababu utakatifu ni wa wale wanaotaka utakatifu kwa imani yao wenyewe bila kuzingatia nini Mungu anachasema katika neno lake.

14. Yesu alipoulizwa na wanafunzi wake, kwa nini alikuwa akisema nao kwa mifano alimnukulu nabii Isaya akisema,:

A. Kusikia mtasikia wala hamtaelewa, Kulia mtalia lakini mtafutwa machozi, kuimba mtaimba lakini hamtasikika, Kusali mtasali lakini sala zenu hazitasikika.

B. Kutazama mtatazama wala hamtaona, kusikia mtasikia wala hamtaelewa, kwa masikio hamsikii vema na macho yao wameyafumba. Wasije wakaona kwa macho wakasikia kwa masikio, wakaelewa kwa mioyo yao.

C. Wakaongoka ni kawaponya, Kusikia mtasikia wala hamtaelewa, kutazama mtatazama wala hamtaona, kwa masikio hamsikii vema na kwa macho yao wameyafumba. Wasije wakaona kwa macho .

15. Ufunguo wa kupata hazina hii ni katika maandiko yafuatayo:
A. Zaburi 119: 110, Zaburi, 11: 23
B. Zaburi 1:1-3 , Zaburi 119: 97-104
C. Zaburi 1: 3, Zaburi 119: 104

16. **Andika Dondoa moja ya zile tofauti na lile mara ya kwanza**:

HERMANUITIKSI
MTIHANI WA TATU
MWAKA 2001
MHULA 1
MKUFUNZI: Francis Wechesa
JINA LA MWANAFUNZI_____20/07/2001

1. Mtu anapoamua kujitunzia hazina yake mbinguni jicho lake huwa na kusudi moja na mwili wake mzima huwa umejaa nini?

A. Nuru B. Giza C. Uhai

2. Mtu anayetafuta hazina ya muda mfupi ya dunia hii, macho yako ni maovu na mwili mzima umejaa nini?

A. Nuru B. Giza C. Uzima

3. Je, kutokana na 2Pt. 1:20-21 ni vigumu sana kwa mwanadamu kuitafsiri Biblia?

A. Ndiyo B. Hapana C. A & B yote makosa

4. Kwa nini Paulo katika Mdo. 20:26,27 amedai kwamba hakuwa na hatia na damu watu wote?

A. Kwa sababu alikuwa mtume B. Kwa sababu alikuwa amefundisha kusudi lote la Mungu
D. Kwa sababu wayahudi walikuwa wamemchukia.

5. Biblia ina jumla ya vitabu vingapi?_____Agano la kale lina_____
Agano Jipya lina_____

6. Mojawapo ya sababu watu wengi huona biblia kuwa ngumu kusoma ni kwa sababu hawana ufahamu kuhusiana na vipindi vingapi?_____

7. Kati ya vipindi vile zaidi ya kumi ta vipindi saba.

1._____2._____

3._____4._____

5._____6._____

7_____

8. Andika madondoa mawili ambayo unajua hujawahi kuyafanya katika mtihani

ARUSHA BIBLE SCHOOL

HERMANIUTIKSI MTIHANI WA MWISHO

MWAKA WA 2001

MHULA WA TATU

JINA LA MWANAFUNZI_____5TH.OCT. 2001

I. Chagua jibu sahihi:

1. Kitu kilicho sahihi katika maisha, kikifananishwa na kuleta maana ya k iroho huitwa:
A. Ngano B. Mithali au mfano C. Hadithi au Metofa

2. Kuwaficha ukweli wasio waaminifu ni moja wapo ya sababu ya kutumia nini?
A. Lugha halisi B. Mithali au mfano C. Mahubiri

3. Jumla nyaraka za Agano hazikufuata namna fulani ya jina la mwandishi, mwandikiwa, Salamu, shukurani, na Mwili na Salamu za mwisho.
A. Kweli B. Uongo, C. A na B zote ni makosa

4. Waraka wa Agano Jipya ulioandikwa ili kuwashawishi Wayahudi k wamba, injili ndiyo ukamilifu wa sheria uliitwa waraka kwa:

A. Wakorintho, B. Warumi C. Waebrania

5. Waraka wa Agano Jipya ulioandikwa ili kusaidia kurekebishi fundisho la uongo walilolifundisha wandugu walioka katika dini ya Kiyahudi waliotaka kuwalazimisha wakristo kushika sheria na kutahiriwa uliitwa waraka kwa:
A. Waefeso B. Wagalatia C. Waebrania

6. Waraka kwa Wakolosai unalenga: A. Kristo na wanafunzi wake B. Kristo na kanisa

lake na ukuu wake Kristo C. Kristo na Ukristo na ukuu wake Kristo

7. Warala unaolenga Kanisa la Kristo ni: A. Wakolosai B. Efeso C. Rumi

8. Waraka uliokusudiwa kumsihi Timotheo kupigana vita vizuri ulikuwa ni:

A. Tito B. 1Timotheo C. 2Timotheo

9. Waraka uliokudiwa kumtia nguvu Timotheo asitahayarike ni:
A. 1Wathesolonike B. 2Timotheo C. 1Timotheo

10. Filemoni ni waraka uliojaa upendo kutoka kwa nani? A. Onesimo B. Paulo C. Dema

11. Waraka uliokusudiwa kuelezea maisha ya mkristo katika vitendo ni:
A. Yuda B. Yakobo C. Ufunuo

12. Waraka uliokusudia kusaidia kuvumilia majaribu yanayotujia ni:
A. 1Wakorintho B. 1 Petro C. 2Petro

13. Waraka 1Yohana unaelezea matatizo ya nani? A. Deotrofe B. Dema
C.Mpinga Kristo.

14. Mojawapo ya sifa ya maandiko ya siri yenye kanoni :
A. Ujumbe zaidi hutolewa kwa njia ya maono B. Huwa ndefu C. Haieleweki

15. Zaburi zenye sala zinazoelekezwa moja kwa moja kwa Mungu na mtu au kikundi cha watu hasa wakati wa mahangaiko huitwa.
A. Zaburi za shukurani B. Zaburi za sifa C. Zaburi za maombolezo

16. Zaburi zinazotolewa hadharani na yule au waabudu wengi wakitambua matendo ya Mungu ya uaminifu kwa niaba ya watu wake katika siku za nyuma, au kuonyesha uhakika wao katika matendo ya siku zijazo huitwa:
A. Zaburi za laana B. Zaburi za shukurani C. Saburi za maombolezo

17. Mashairi ya kuelekeza uchungu wa haki wa mtunga zaburi kwa maadui wa Mungu akitaka kisasi cha Mungu kitolewe haraka huitwa :
A. Zaburi za Kifalme B. Zaburi za maombolezo C. Zaburi za laana.

18. Katika usambamba wa Kiebrania kuna vina vingapi utakavyoweza kukutana navyo?

A. Vinne B. Vitano C. Vingi sana

19. Usambamba ambao wazo katika msitari wa kwanza hurudiwa katika msitari wa pili huitwa:
A. Ya kilicho kinyume B. Yenye maana moja C. Ya kufanywa

20. Usambamba ambao wazo katika msitari wa kwanza huwekwa kinyume na msitari wa pili. A. Yenye mfano B. Ya kilicho kinyume C. Yenye maana moja

21. Usambamba wenye wazo la msitari wa pili hupanua na kutilia nguvu wazo katika msitari wa kwanza. Huitwa . A. Yenye mfano B. Ihusuyo tabia ya nchi. C. Ya kufanywa.

ARUSHA BIBLE SCHOOL

HERMANUITIKSI(ELIMU YA KUFASIRI)

MTIHANI WA MWISHO

JINA_____

Mkufunzi: Francis Wechesa

JIBU NDIYO AU HAPANA

1._____Kanuni ya kimsingi haiwezi kutumika kwa matumizi tofauti.

2._____Paulo alitumia kanuni hii ya kimsingi kuhusu mambo ya fedha.

3._____ Yesu alitumia neno la mavuno akizungumzia roho za wanadamu wasio taka kusikia injli.

4._____Kanuni ya kimsingi inafungwa na Agano husuka.

5._____Kanuni ya kimsingi haibadiliki isipokuwa inaweza kubadilishwa.

6._____Katika ulimwengu wa maumbili(sheria ya asili) kila kitu kinabadilika.

7._____Kanuni ya kimsingi zinazofundishwa katika Warumi 16:16 kuhusiana na busu takatifu ni kwamba hata leo ni dhambi tusiposalimiana kwa busu.

8._____Katika karne ya kwanza salamu zao zilikuwa busu kwenye shavu.

9._____Katika mfano ya Bwana wa kuwatawadha wanafunzi wake miguu ni fundisho kwamba hata leo wanafunzi wa Yesu wanapaswa kutawadhana miguu.

10_____Wanafunzi wa Yesu hawapaswi kuhudumiana ingawa Bwana aliwahudumia kwa unyenyekevu.

11_____Katika 1Wakorintho 11:2-16 kuna kanuni ya kimsingi inayoweza kufahamika ingawa ni moja ya mafungu ya maandiko magumu.

12._____Mojawapo ya njia za uhakika kuhusu kuanzisha habari za vitendo au fundisho kuwa linawahusu watu wa siku hizi kinyume na tamaduni zao, ni kuona ikiwa inashikamana na kile kinachojulikana na wengine kama “taratibu za muumbo”

13_____ Katika fundisho la mwanamume kuwa kichwa cha mwanamke Paulo anashikamanisha fundisho la kale lisilohusiana na tamaduni za watu.

14._____Fundisho hili linasema, mwanamume ndiye aliyeumbwa kwanza, na mwanaume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamke.

15_____Katika fundisho la Paulo anatuelezea kwamba Adamu ndiye aliyedanganywa.

16._____Mifano inayotufunga na amri ya moja kwa moja kutoka kwa Mungu, daima huwa na baadhi na yasiyoya lazima.

17._____Katika Matendo ya Mitume 10:47-48 amri hii ya “kubatizwa” ilikuwa ya lazima na kiasi cha joto cha maji nacho kilikuwa cha lazima.

18._____Kutokana na amri hii ya kubatizwa maji yalitakiwa kuwa maji yanayokwenda.

19._____Kumbatizia mtu katika kisima ndani ya jengo ingelikuwa kuvunja amri ya Mungu ya ubatizo.

20_____Isiyo ya lazima inaweza kuwako kutusaidia kutekeleza iliyo ya lazima.

21._____Katika amri ya Mungu ya kuimba hakuna yasiyo ya lazima katika utekelezaji wa amri hiyo.

22._____Kutumia kitabu cha nyimbo katika utekelezaji wa amri ya Mungu ya kuimba ni uasi.

23._____Kutumia sehemu nne za nyimbo zenye kukubaliana ni mojawapo wa ile isiyo ya lazima.

24_____Washiriki wa kanisa la Kristo ili wapate kutekeleza amri ya Mungu ya kuimba, wanapaswa kuimba nyimbo zilizotungwa na wahubiri na wazee wa kanisa tu.

25_____Katika utaratibu wa ibada, ili kutekeleza amri ya Mungu ya kuimba, tunapaswa kuimba kabla ya sala.

26_____Watu wakiimba kwa sauti zenye mpangilio wa Soprano, Alto, Tenor, bass ni kwaya kwa hiyo ni dhambi.

27_____Kujaribu kufanya amri ya Mungu inayohusu –ote kuwa ile inayohusu watu , kitu, wakati maalumu ni kuzuia neno la Mungu

28_____Kujaribu kufanya amri ya Mungu inayohusu watu,kitu, wakati, maalumu kuwa ya – ote, ni kupotosha neno la Mungu.

29_____Katika amri ya Agizo kuu (Mathayo 28:18-20, Marko 16:15, Luka 24:44-49) haina amri inayohusu –ote.

30_____Enendeni ni amri inayohusu maalum.

31._____Katika amri ya k uenenda, tunapaswa kufuata mfano wa vyombo Yesu na Mitume walivyovitumia katika kuenenda.

32._____ “Fanya wanafunzi” au “fundisha” au “Hubiri” injili inahusu somo lenyewe, kwa hiyo ni amri “maalumu”.

33._____Baptizo katika neno la Kiyunani ni “nyunyiza”

34._____Rantizo katika neno la Kiyunani ni “Tosa”

35._____Kumwagia katika Kiyunani ni “ekcheo”

36._____Katika Mdo.8:35-39 na 10:47,48 kutosha ni katika “Roho Mtakatifu”

37._____Amri ya kutosa si amri ya kimitume.

38_____Kuimba ni mojawapo ya amri ya maalumu.

39._____Kuna aina mbili ya muziki.

40._____Kuimba ni kufanya muziki lakini si kila kufanya muziki ni kuimba.

41._____Muziki wenye maneno ndiyo kuimba.

42._____Kupiga vyombo vya muziki si kuimba bali ni kufanya muziki.

43._____Tukiimba na kupiga vyombo vya muziki tunafanya aina mbili ya muziki.

44._____Neno la Kiyunani “Ado” ni kusifu Mungu.

45._____Mungu aliposema katika Agano Jipya tuimbe alikuwa akikataza aina nyingine ya muziki.

46._____Mungu katika kitabu cha Mwanzo alimwagiza Nuhu kujenga Safina akitumia mti wa mvinje.

47_____Kama angelitumia mti mwingine pamoja na mvinje angelimpendeza Mungu tu.

48._____Nuhu alikuwa na hiari ya kutumia saizi yoyote ya mti wa mvinje katika utekelezaji wa amri ya Mungu ya kujenda Safina.

49._____Msonobari katika ujenzi wa Safina ungelikuwa nyongeza.

50._____Mti ulikuwa ni aina maalumu ya kifaa tofauti kabisa na chuma au aina nyingine ya kifaa.